# Nipashe

Alhamisi Januari 30, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580141

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital  nipasheTZ  nipasheTZ  nipasheTZ  0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## Bunge laagiza uwekezaji wa hisa Vodacom uchunguzwe

UKURASA 3


ama

AFYA NA MAZINGIRA

Mashabiki soka waongoza msongo, shinikizo

Taasisi ya lishe katika mageuzi kumwondolea mtoto utapiamlo

UKURASA 13

# Serikali yajizatiti kuikabili corona



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu.

• **Yatangaza** upimaji wanaoingia nchini, kambi tatu za udhibiti zawekwa hadharani...

*Endelea ukurasa 2*


## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**LITA 7,000 ZA DAWA KUPAMBANA NZIGE**

SERIKALI imetenga lita 7,000 za dawa ya viuatilifu kwa ajili ya kupambana na wadudu aina ya...

UKURASA WA 7

**280,000 WAPATA PASI MPYA ZA KIELEKTRONIKI**

IKIWA imesalia siku moja ili serikali isitishe matumizi ya hati za zamani za kusafiria, idadi ya waliojitokeza...

UKURASA WA 24

**BENKI AZANIA YAWAPA FURSA W'SHARA WADOGO**

BENKI ya Azania imeendelea kuwapa fursa mbalimbali wafanyabiashara wadogo, baada ya jana...


## Mafundi wa simu wapewa kibano

UKURASA 3

## Akamatwa kwa tuhuma kujifanya usalama wa taifa

UK.2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play  App Store



MICHEZO **SAMATTA ATUSUA, APEWA BAO** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

## Lita 7,000 za dawa kupambana na nzige

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imetenga lita 7,000 za dawa ya viuatilifu kwa ajili ya kupambana na wadudu aina ya nzige endapo wataingia nchini.

Wadudu hao kwa sasa wapo Kenya na walianzia Ethiopia, wamekuwa wakishambulia kwa haraka mazao na kusababisha uharibifu mkubwa.

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa, alisema nchi iko salama na kwamba nzige hao hawajaingia nchini.

Alisema serikali imeshatenga kiasi hicho cha dawa kwa ajili ya kuwaua nzige hao endapo wakiingia nchini.

"Tumetenga kiasi hicho cha dawa ambapo lita moja ina uwezo wa kukabiliana na hekta moja," alisema Hasunga.

Alisema makundi ya nzige wa jangwani yameonekana eneo la Karamoja umbali wa kilomita 166 kutoka mpaka wa Uganda.

Alisema kundi moja lina uwezo wa kuruka bila kutua kwa umbali wa kilomita 150 kwa siku na nzige mmoja anauzito wa gramu mbili, uwezo wa kula sawa na uzito wake kwa siku.

Aliongeza kuwa kundi moja la nzige linakadiriwa kufika milioni 40 kwenye eneo la kilomita moja za mraba na lina uwezo wa kusababisha upotevu wa uoto takribani tani 80 kwa siku katika eneo hilo.

Alisema nzige hao wamesharipotiwa katika nchi za Eritrea, Ethiopia, Somalia Sudan na Kenya.

Waziri Hasunga aliwataka Watanzania kutokuwa na wasiwasi kwa sababu serikali imejipanga kwa ajili ya kukabiliana na nzige hao ambao ni hatari. Alisema kuna hatua mbalimbali ambazo zinachukuliwa na serikali kila mwaka na kwamba hutenga fedha kwa ajili ya kukabiliana na nzige endapo watatokea katika maeneo hayo.

Alisema wizara imewatuma wataalamu katika mikoa ambayo iko jirani na mipakani ili kuhakikisha nzige waliopo nchi jirani hawaingii nchini.

Alisema wameandaa mpango wa kukabiliana na nzige hao kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za serikali, mashirika ya kimataifa na sekta binafsi huku waliendelea kutoa elimu ya utambuzi na udhibiti kwa wadau wa kilimo wakiwamo na maofisa ugani katika maeneo mbalimbali nchini.

Alisema wananchi wanapaswa kutoa taarifa ya viashiria au uwapo wa nzige kwenye maeneo ya kilimo malisho na uoto wa asili.

Alisema wakulima wanapaswa kutoa ushirikiano kwa wataalamu wa wizara ya kilimo katika hatua mbalimbali za tahadhari na udhibiti wa nzige endapo watatokea.

Waziri Hasunga alizitaka sekretieti za mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwasimamia maofisa ugani kuhakikisha wanatembelea wakulima mashambani.

# Serikali yajizatiti kuikabili corona

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

KASI ya virusi vya homa kali ya mapafu duniani vinavyosababishwa na kirusi aina ya corona, imesababisha serikali ya Tanzania kutenga maeneo matatu maalum kwa ajili ya kujiandaa na matibabu ya washukiwa wa mlipuko wa ugonjwa huo iwapo watajitokeza.

Maeneo yaliyoandaliwa kwa matibabu na kupokea washukiwa hao ni Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro (Mawenzi), Hospitali ya kudhibiti magonjwa ambukizi ya Buswelu ya Mwanza na Hospitali ya Kigamboni, jijini Dar es Salaam.

Jana, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, akitoa taarifa kuhusu mwenendo wa ugonjwa huo ulioikumba China na mataifa mengine duniani, alisema kuna washukiwa walioripotiwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika ambao wamegunduliwa Kenya, Zimbabwe, Ivory Coast, Ethiopia na Mauritius.

Alisema serikali itatoa taarifa rasmi baada ya uthibitisho kufanyika, ingawa nchini hadi sasa hakuna mgonjwa wala mtu yeyote aliyehisiwa kuwa na ugonjwa huo.

"Serikali kupitia Wizara ya Afya imechukua hatua zifuatazo katika kukabiliana na tishio la ugonjwa huu. Tumeanza kufanya uchunguzi wa wasafiri wote kutoka Bara la Asia kwenye mipaka yetu ikiwamo viwanja vya ndege vya Mwalimu Julius Nyerere (JNIA), Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), Mwanza na Bandari ya Dar es Salaam.

"Kwa mfano kwa kipindi cha wiki mbili ziizopita, tumefanya uchunguzi kwa wa raia 1,520 walioingia nchini wakitokea China na Asia kupitia mipakani na viwanja vya ndege. Tumeanza kufanya uchunguzi wa abiria wa ndege zote zinazoingia nchini."

Kwa mujibu wa Ummy, wizara hiyo tayari inavyo vipima joto 140 vya mkono 125 na vya kupima watu wengi kwa mpigo 15, ambavyo vimefungwa na vinatumika katika maeneo mbalimbali ya mipakani ikiwamo viwanja vya ndege na bandari. Ugonjwa huo umekuwa ukisambaa kwa kasi ambapo kumekuwa na ongezeko la wagonjwa pamoja na vifo katika kipindi kifupi kwa wastani wa zaidi ya wagonjwa 200 kwa siku. Aidha, alisema wizara hiyo inaendelea kuchukua na kupima sampuli kutoka maeneo ya ufuatiliaji na yeyote atakayehisiwa kuwa na dalili za ugonjwa huo, sampuli zitafikishwa kwenye maabara ya Taifa na kupimwa.

Kutokana na tahadhari hiyo, Waziri Ummy alisema mpaka sasa watumishi wa sekta ya afya 2,297 wameshapatiwa mafunzo ya kukabiliana na magonjwa ya mlipuko na majanga ikiwamo jinsi ya kutoa matibabu ya magonjwa ya mlipuko, kuchukua sampuli, uelimishaji na kufuata kanuni za afya.

Ugonjwa huo unaosababishwa na kirusi jamii ya corona na ni kipya 'Novel (New) Corona virus 2019'ambacho ni tofauti na virusi vingine vya jamii hiyo ambavyo viliwahi kusababisha milipuko ya ugonjwa unaojulikana kama 'Sars-Cov' mwaka 2003 na Mers-Cov Corona Virus mwaka 2013.

Inaelezwa kuwa ugonjwa huo huambukizwa kwa njia ya hewa kwa kuingiwa na majimaji yenye virusi kutoka kwa mtu mmoja kwa njia ya kukohoa au kupiga chafya au kwa kugusa majimaji au makamasi kutoka kwa mgonjwa aliyethibitishwa kuwa na dalili za ugonjwa huo.

Kwa mujibu wa Waziri Ummy, dalili za ugonjwa huo huanza kuonekana kati ya siku moja hadi 14 tangu kupata maambukizo.



Mtumishi wa kampuni ya utalii ya Coastal Fanjove Ltd, inayojihusisha na shughuli za utalii katika Kisiwa cha Fanjove, Kata ya Songo Songo, wilayani Kilwa, mkoani Lindi, Kudeme Hakimu, akiwasaidia kuwarejesha baharini samaki sita aina ya Dolphine, waliosukumwa na maji ufukweni juzi. **PICHA: SAID HAMDANI**

# Abambwa kwa kujifanya usalama wa taifa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga linamshikilia mkazi wa Shinyanga mjini, Sheliku Sweya (45), kwa tuhuma ya kujifanya ofisa usalama wa Taifa, kutapeli fedha watumishi wa umma, kuomba rushwa ya ngono.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Deborah Magiligimba, alisema mtuhumiwa huyo kwa nyakati tofauti amekuwa akitembelea ofisi za umma na kuanza kutapeli watumishi na kwamba alifanikiwa kumtapeli Mganga wa Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga, Geofrey Mboye, kiasi cha Sh. 300,000.

Kamanda Magiligimba alisema mtuhumiwa huyo alifika kwenye hospitali hiyo na kuonana na mganga huyo na kujitambulisha kuwa ni ofisa usalama wa Taifa na atamsaidia shida zake. "Ndipo akamwambia amsaidie kumhamisha kutoka Shinyanga kwenda Dodoma na kuombwa kiasi hicho cha fedha na kutapeliwa," alisema Kamanda Magiligimba.

Alisema mtuhumiwa huyo hakuishia hapo pia alikwenda kwa Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Rose Malisa, ambaye alimuomba rushwa ya ngono kwa ahadi ya kumtatulia changamoto zilizopo hospitalini hapo, ikiwamo kupatiwa vifaa tiba pamoja na kuongezewa watumishi wa afya.

"Mtuhumiwa alimuahidi mganga huyo kuwa atamfutia deni analodaiwa na taasisi ya afya alikopata masomo ya udaktari wa magonjwa bingwa ya kinamama kiasi cha Sh. milioni 40 ndipo akamshitukia na kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi na kuwekewa mtego na kufanikiwa kukamatwa," alisema Magiligimba.

Alisema baada ya mganga huyo kuwa na shaka, alitoa taarifa Jeshi la Polisi ambalo liliweka mtego wa rushwa hiyo ya ngono, na kabla ya mtuhumiwa kufanikiwa kupata rushwa hiyo alikamatwa.

Alisema walipofanya uchunguzi walibaini kuwa siyo ofisa usalama wa Taifa.

Kamanda Magiligimba alisema Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi juu ya mtuhumiwa huyo, upelelezi ukikamilika, atafikishwa mahakamani.

## HABARI KITAIFA



Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara wa Benki ya Azania, Rhimo Nyansaho, (kushoto), Mwenyekiti UWT Taifa, Gaudensi Kabaka, Mhandisi Julius Ndyamukama, Mkurugenzi Mkuu wa benki hiyo, Charles Itembe na Mbunge wa Geita Vijijini, Joseph Kasheku "Msukuma" wakishuhudia wakati Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula, akikata utepe kuzindua akaunti ya mikopo ya Jikwamue, katika hafla iliyofanyika jijini Mwanza jana. Habari Uk. 24. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uwekezaji NSSF hisa za Vodacom kuchunguzwa

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

BUNGE limeitaka serikali kufanya uchunguzi wa kina kuhusu uwekezaji wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) katika hisa za Vodacom kutokana na kutozingatiwa mwongozo wa uwekezaji wa mifuko ya hifadhi ya jamii.

Azimio hilo la Bunge lilitolewa jana na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Naghenjwa Kaboyoka, wakati akisoma Bungeni taarifa ya shughuli za kamati hiyo kwa mwaka 2019.

Alisema kwa kuwa uchambuzi wa kamati katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ulibaini kuwa uwekezaji wa NSSF katika hisa za Vodacom haukuzingatia mwongozo wa uwekezaji wa mifuko ya hifadhi ya jamii, Bunge linaazimia kwamba serikali ifanye uchunguzi wa kina wa suala hilo na kuchukua hatua stahiki kwa kuzingatia matokeo ya uchunguzi.

Kaboyoka alisema uwekezaji uliofanywa na NSSF katika hisa za Vodacom unaotoa faida ndogo kulinganisha na dhamana za serikali.

Pia alisema mwongozo wa uwekezaji katika mifuko ya hifadhi ya jamii unaelekeza kwamba mifuko iwekeze katika maeneo ambayo faida zake ni kubwa kuliko hati fungani (dhamana) za serikali.

Aidha, alisema kwa maeneo ambayo faida yake ni ndogo kuliko dhamana za serikali, mfuko husika utatakiwa kupata idhini ya Benki Kuu ya Tanzania (BOT) kabla ya kuwekeza katika maeneo hayo.

"Taarifa ya CAG imebainisha kuwa Aprili 5, 2017, NSSF iliomba ridhaa ya BOT ili kuwekeza katika hisa za Vodacom ambazo faida yake ilikuwa chini ukilinganisha na dhamana za serikali," alisema.

Alisema endapo NSSF wangewekeza kwenye dhamana za muda mfupi zingetoa faida ya asilimia 15 na zile za muda mrefu kwa miaka mitano zingetoa faida kwa asilimia 17.92

Kuhusu uwekezaji usio na tija uliofanywa na NSSF, Kaboyoka alilieleza Bunge kuwa serikali ilifahamisha kamati yake kuwa miradi yote iliyotekelezwa na shirika hilo na kuwa na dosari katika utekelezaji wake, ipo chini ya uchunguzi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru).

**MIKOPO YA TIB**

Kuhusu mikopo chechefu katika Benki ya Maendeleo ya TIB, Mwenyekiti huyo alisema serikali imetoa ufafanuzi kuwa wakopaji waliochukua jumla ya Sh. bilioni 89 walipewa notisi ya kutakiwa kurejesha mikopo yao kama Bunge lilivyoazimia.

"Changamoto kubwa kwa suala la mikopo chechefu ni kuwa wakopaji wanakimbilia mahakamani na kuomba zuio la mali zao kukamatwa, hivyo kukwamisha jitihada za urejeshaji wa mikopo kupitia dhamana za wadaiwa," alieleza Kaboyoka.

**DENI TBA PASUA KICHWA**

Kuhusu deni ambalo Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) walikuwa wamechukua mkopo katika Benki ya CRDB na kuonekana uwepo wa vipengele vyenye masharti hasi kwa serikali, kamati hiyo imelieleza Bunge kwamba imefahamishwa kuwa mkopo husika wa Sh. 3,626,896,766 umesitishwa kama Bunge lilivyoazimia.

Aidha, Kaboyoka alilieleza Bunge kuwa 'commitment fee' ya asilimia mbili ambayo ilikuwa moja ya sharti hasi katika mkopo huo ilisitishwa.

**TRA YAGUSWA**

Katika taarifa hiyo ya Kaboyoka, Bunge limeelezwa kuwa pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) katika kukusanya mapato ya serikali, uchambuzi wa kamati katika taarifa ya CAG kwa hesabu zinazoishia Juni 30, 2018, umebaini changamoto kadhaa za ambazo zinapunguza kasi ya ukusanyaji

INAENDELEA UK. 8

# TCRA yawapa kibano mafundi wa simu

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Kanda ya Kaskazini imetangaza kibano kwa mafundi wa

vifaa vya kielektroniki zikiwamo simu za mkononi kwamba wale wasiosajiliwa hawataruhusiwa kufanya kazi hiyo.

TCRA imesema kibano hicho kitaanza Julai, mwaka huu, na kwamba hakuna fundi ambaye atafanya kazi kama hajasomea wala kusajiliwa hivyo ni muhimu kujiunga kwenye kikundi ili kupatiwa elimu.

Mwanasheria wa TCRA, Kant Mosha, alisema hayo juzi katika mkutano wa mafundi wa vifaa vya kielektroniki uliofanyika kwenye ukumbi wa ofisi ya mkuu wa mkoa wa Arusha.

Mushi aliwataka mafundi hao kuwa na usajili wa kikundi na hilo ndilo suluhisho.

Alisema mafundi simu ni kada ambayo ilikuwa imesahauliwa lakini kuanzia sasa, serikali

imeamua kuwatambua, hivyo kuungana ni sehemu ya kufanikiwa kwa malengo yao.

Mwenyekiti wa Chama cha Mafundi Simu Kanda ya Ziwa, Maguwa Manyanda, aliwataka kutambua kwamba mafundi simu ni wa thamani kwa kuwa jamii inawategemea na wanachangia mapato ya serikali.

Kutokana na hali hiyo, alisema ni muhimu kuona umoja ndio suluhisho la changamoto zao.

Alisema mafunzo hayo yataondoa changamoto na kuwafanya kuwa huru katika shughuli zao za kila siku, hivyo umoja ni nguzo ya kuwafikisha kushirikiana na serikali katika masuala mbalimbali vikiwamo vyombo vya dola.

Manyanda alisema ili kila moja atende kazi zake ni muhimu akajiunga na umoja ili kuondoa changamoto zao ambazo zimekuwa zikiwafanya kukumbana na misukosuko kutoka polisi.

Naye Mwenyekiti wa Umoja wa Mafundi Simu Kanda ya Kaskazini, Nasri Mtengeti, alisema wamefurahi kupata elimu hiyo ya umoja ambayo itawasaidia kuondokana na changamoto mbalimbali.

Awali, akitoa mafunzo kwenye mkutano huo, Mratibu wa Vikundi hivyo kutoka TCRA, Mhandisi Kadaya Buluhye, aliwataka mafundi hao kufanya kazi kwenye umoja kwa lengo la kupata elimu na usajili.

Alisema Jeshi la Polisi linafanya kazi ya kulinda usalama na mali za raia, lakini umoja wao utasaidia kufanya kazi kwa karibu na jeshi hilo na kuondoa changamoto ambazo wamekuwa wakikumbana nazo kama mafundi.

NHC
SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA
TUNAJENGA TAIFA LETU

## TAARIFA KWA UMMA

Shirika la Nyumba la Taifa linapenda kuwatangazia wapangaji wake wote wenye malimbikizo na waliohama na madeni wakiwamo watu binafsi, taasisi za umma, wakala za serikali na kampuni binafsi kulipa malimbikizo na madeni hayo katika kipindi cha siku 14 kuanzia tarehe ya tangazo hili na watakaoshindwa kufanya hivyo katika muda uliopangwa hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao. Shirika litawatangaza wadaiwa SUGU wote kwenye vyombo vya habari.

Kwa wale wanaofahamu kwamba upangaji wao ulipatikana kwa njia zisizo sahihi wanapaswa kutoa taarifa Makao Makuu ya Shirika ili kuweza kurasimishwa.

***Epuka usumbufu lipa kodi kwa wakati.***

**Imetolewa na:**

**OFISI YA MAWASILIANO KWA UMMA NA HUDUMA KWA JAMII**
**NHC- MAKAO MAKUU**

# TANGAZO



## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
*benki kwa maendeleo yako*

### AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.12.2019
### (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka Mwaka wa sasa 31-Dec-19 | Robo Mwaka Mwaka uliopita 30-Sep-19 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 10 317 | 9 197 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 15 679 | 9 893 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 25 670 | 25 470 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 211 | 104 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 22 | 122 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 0 | 0 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 84 597 | 91 576 |
| 12 | Mali Nyingine | 12 886 | 13 890 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 20 | 20 |
| 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2 451 | 2 766 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **151 852** | **153 037** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 3 361 | 1 924 |
| 18 | Amana za Wateja | 107 111 | 109 315 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana Maalumu | 0 | 0 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0 | 0 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 2 | 3 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 3 626 | 4 519 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 4 | 12 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 822 | 1 171 |
| 27 | Dhima Nyingine | 1 324 | 1 239 |
| 28 | Madeni | 12 086 | 13 001 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **128 337** | **131 183** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **23 514** | **21 853** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 10 985 | 8 607 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 6 728 | 7 549 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 232 | 496 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 5 570 | 5 202 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **23 514** | **21 853** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 372 | 280 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 16 706 | 19 848 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 9 353 | 12 274 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 1 461 | 1 459 |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 15.5% | 14.3% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 17.6% | 18.9% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 84.6% | 92.3% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 62.3% | 68.7% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 72.8% | 76.5% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -0.7% | -0.7% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -0.8% | -1.8% |

### AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI
### KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.12.2019
### (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 31-Dec-19 | Robo ya mwaka Linganishi 31-Dec-18 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-19 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 31-Dec-18 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 7 770 | 6 948 | 29 265 | 28 721 |
| 2 | Gharama za Riba | -1 526 | -1 150 | -5 421 | -5 385 |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **6 244** | **5 798** | **23 844** | **23 336** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | -918 | -160 | -2 321 | -3 056 |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **1 379** | **1 749** | **6 559** | **7 987** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 97 | 16 | 349 | 90 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 867 | 1 446 | 4 845 | 7 077 |
| | 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 416 | 287 | 1 366 | 819 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **-7 083** | **-7 011** | **-27 750** | **-31 994** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | -3 541 | -3 130 | -14 083 | -16 000 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | -3 542 | -3 881 | -13 667 | -15 994 |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **-377** | **376** | **331** | **-3 727** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 113 | 0 | -99 | 1 187 |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **-264** | **376** | **232** | **-2 540** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **-264** | **376** | **232** | **-2 540** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 427 | 450 | 427 | 543 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | -24 | 44 | 21 | -295 |
| 15 | **Idadi ya Matawi** | **18** | **18** | **18** | **18** |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -0.7% | 1% | 0.2% | -4% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -4.7% | 7% | 1.0% | -25% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 92.9% | 93% | 91.3% | 92% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 21.9% | 21% | 20.9% | 16% |

### AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31.12.2019

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2019** | **8 607 136** | **2 431 917** | **7 546 745** | **2 537 257** | **779 217** | **21 902 272** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 231 847 | 0 | 0 | 231 847 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| Miamala na wanahisa | 2 377 395 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 377 395 |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | (1 598 279) | 601 041 | 0 | (997 238) |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 779 217 | 0 | (779 217) | - |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2019** | **10 984 531** | **2 431 917** | **6 959 530** | **3 138 299** | **-** | **23 514 276** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2018** | **8 607 136** | **2 431 917** | **12 981 019** | **694 193** | **843 314** | **25 557 579** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | -3 787 365 | 0 | 0 | -3 787 365 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | -3 336 159 | 3 304 680 | 0 | -31 478 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 64 097 | 0 | -64 097 | 0 |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2018** | **8 607 136** | **2 431 917** | **5 921 593** | **3 998 873** | **779 217** | **21 738 735** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA
### KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31.12.2019
### (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 31-Dec-19 | Robo Mwaka iliyopita 30-Sep-19 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-19 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 31-Dec-18 |
|---|---|---|---|---|---|
| **I:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | -377 | 178 | 331 | -3 727 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | - Hasara Katika Mali | 358 | 338 | 1 497 | 1 552 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 6 979 | -1 605 | -1 601 | 17 320 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | -0 | 0 | 3 | -103 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | -768 | -874 | -8 346 | -31 969 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | -200 | -2 255 | 1 195 | -6 965 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | -2 079 | -1 780 | 3 137 | 7 812 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 792 | -211 | -309 | 922 |
| | - Kodi Iliyolipwa | -163 | -0 | -338 | 0 |
| | - Mengineyo (bainisha) | 117 | 1 165 | 1 660 | 2 367 |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | **4 660** | **-5 044** | **-2 771** | **-12 792** |
| **II:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | -2 | 81 | -427 | -1 023 |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | -4 | 2 | 2 | 76 |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mengineyo (bainisha) | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | **-6** | **82** | **-425** | **-947** |
| **III:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 2 377 | 0 | 2 377 | 0 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | -1 | -1 | -2 | -1 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mengineyo (bainisha) | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **2 377** | **-1** | **2 376** | **-1** |
| **IV:** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 7 030 | -4 963 | -821 | -13 739 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 11 735 | 16 697 | 19 585 | 33 325 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **18 765** | **11 735** | **18 765** | **19 585** |

**BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.12.2019**

Katika kuanda taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

| ***Jina na Cheo*** | ***Saini*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|
| Juliana Swai **(Kaimu Mtendaji Mkuu)** | | |
| Bertha Simon **(Mkuu wa Fedha)** | | |
| Chemo Mutani **(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)** | | |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| ***Jina*** | ***Saini*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|
| 1. Ernest Massawe | | |
| 2. Dr. Josephat Daniel Lotto | | |




215605102

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Tahadhari dhidi ya corona izingatiwe*

**HOMA** itokanayo na virusi vya corona imekuwa tishio kwa sasa duniani kote, baada ya kulipuka nchini China na kusambaa kwa kasi kubwa katika mataifa ya jirani.

Ugonjwa huo ni tishio kwa kuwa licha ya kuambukuza watu kwa kasi, pia unaua haraka, na tayari umesababisha vifo kadhaa nchini China.

Kuna taarifa, ambazo hata hivyo hazijathibitishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO), kwamba kuna mataifa kadhaa yakiwamo ya Bara la afrika ambayo raia wake wanashukiwa kuathirika.

Kutokana na hali hiyo, kuna umuhimu kubwa wa kuchukuliwa hatua na mamlaka zetu za kudhibiti uwezekano wa kuingia kwa ugonjwa huo nchini kwa lengo la kulinda usalama wa taifa letu na watu wake.

Tunasema hivyo kwa kuwa athari za magonjwa ya mlipuko ni tishio kubwa kutokana na uzoefu uliopo kwa baadhi ya magonjwa hayo kama ebola na mengineyo, ambayo yamekuwa yakisababisha maafa makubwa kwa baadhi ya nchi.

Kwa kudhihirisha kuwa serikali yetu inalizingatia hilo, jana ilitangaza hatua mbalimbali ikiwamo kutenga maeneo matatu maalum kwa ajili ya kujiandaa na matibabu ya washukiwa wa mlipuko wa ugonjwa huo iwapo watajitokeza.

Maeneo yaliyoandaliwa kwa matibabu na kupokea washukiwa hao ni Hospitali ya Rufani ya mkoa wa Kilimanjaro (Mawenzi), Hospitali ya kudhibiti magonjwa ambukizi ya Buswelu ya Mwanza na Hospitali ya Kigamboni, jijini Dar es Salaam.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, akitoa taarifa kuhusu mwenendo wa ugonjwa huo, alisema kuna washukiwa walioripotiwa na WHO Kanda ya Afrika ambao wamegunduliwa Kenya, Zimbabwe, Ivory Coast, Ethiopia na Mauritius.

Alisema serikali itatoa taarifa rasmi baada ya uthibitisho kufanyika, ingawa nchini hadi sasa hakuna mgonjwa wala mtu yeyote aliyehisiwa kuwa na ugonjwa huo.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Afya imechukua hatua kadhaa za kufanya uchunguzi wa wasafiri wote kutoka Bara la Asia kwenye mipaka ikiwamo viwanja vya ndege vya Mwalimu Julius Nyerere (JNIA), Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), Mwanza na Bandari ya Dar es Salaam.

Alisema kwa kipindi cha wiki mbili zilizopita, wamefanya uchunguzi kwa raia 1,520 walioingia nchini wakitokea China na Asia kupitia mipakani na viwanja vya ndege pamoja na kufanya uchunguzi wa abiria wa ndege zote zinazoingia nchini.

Kwa mujibu wa Ummy, Wizara hiyo tayari inavyo vipima joto 140 vya mkono 125 na vya kupima watu wengi kwa mpigo 15, ambavyo vimefungwa na vinatumika katika maeneo mbalimbali ya mipakani ikiwamo viwanja vya ndege na bandari.

Kadhalika, wizara hiyo inaendelea kuchukua na kupima sampuli kutoka maeneo ya ufuatiliaji na yeyote atakayehisiwa kuwa na dalili za ugonjwa huo, sampuli zitafikishwa kwenye Maabara ya Taifa na kupimwa.

Ni hatua ambazo tunaona kuwa serikali imezichukua muda mwafaka, na kama kutakuwa na umakini katika utekelezaji wake, bila shaka zitasaidia sana kudhibiti uwezekano wa ugonjwa huo kuingia nchini.

Tumaanini kuwa watumishi wa sekta ya afya 2,297, ambao Waziri Ummy alisema wameshapatiwa mafunzo ya kukabiliana na magonjwa ya mlipuko na majanga ikiwamo jinsi ya kutoa matibabu ya magonjwa ya mlipuko, kuchukua sampuli, uelimishaji na kufuata kanuni za afya watawajibika ipasavyo katika kutekeleza majukumu yao.

Tunawashauri wananchi kila mmoja kwa nafasi yake kuhakikisha tahadhari hiyo inazingatiwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# *Kukosekana usafi katika shughuli hizi ni hatari*

Na Sabato Kasika

**KATIKA** maeneo ya mijini, ni kawaida kukuta makundi ya watu wakifanya shughuli mbalimbali, zikiwamo za mamalishe, uuzaji nguo za mitumba, kuchoma viazi, mihogo, mahindi na nyingine nyingi.

Baadhi ya shughuli hizo na hasa za mamalishe, zimekuwa zikiambatana na uchafuzi wa mazingira, hali ambayo ni hatari kwa afya za wahusika, pia wateja na umma kwajumla.

Kinyesi cha binadamu, taka ngumu, maji machafu, ni baadhi ya taka zinazosababisha matatizo ya afya na ndizo, zinazoonekana kwenye maeneo ya shughuli zao.

Lakini, wataalamu wa afya wanasema, usafi wa mazingira ni njia ya kuendeleza afya kwa kuzuia mawasiliano ya binadamu na athari za taka kuleta athari na kumfanya mtu augue

Kutokana na hilo, jamii inashauri kuzingatia usafi wa mazingira kuanzia kuandaa chakula, wakati wa kula, pia kufanya biashara katika mazingira safi, ili kuepuka magonjwa yakiwamo ya mlipuko.

Pamoja na kuwapo kwa maelekezo hayo, kuna wakazi wa mijini ambao imekuwa kawaida kwao kukuta wanafanya biashara katika mazingira machafu, pasipo kujali hatari kwa afya zao.

Vilevile, hivi sasa imekuwa jambo la kawaida kukuta watu wamekaa katika banda la mamalishe wanakula chakula, huku pembeni kuna uchafu kama jalala lenye lundo la uchafu unaotoa harufu kali, ambayo ni hatari kwao.

Inawezekana, wapo wasioona kuwa hilo ni tatizo kukaa kwenye mazingira ya aina hiyo na kuandaa chakula, hawaoni kuwa ni tatizo, kukaa na kula chakula kana kwamba kufanya hivyo ni jambo la kawaida.

Ni muhimu kutambua kuwa usafi wa mazingira unahusu pia udumishaji wa ratiba ya usafi, kwa njia ya huduma kama vile ukusanyaji wa taka na maji machafu na kuwa na sehemu maalum ya kuandalia vyakula.

Sehemu hiyo ya kuandalia chakula, inatakiwa imekaguliwa na kuruhisiwa na mamlaka husika, kwa ajili kuepuka magonjwa ya mlipuko yanayoweza kuwakumba pamoja na wateja.

Ikumbukwe kuwa usafi wa mazingira kwenye maeneo ya biashara kama hiyo ya mamalishe, ni unasaidia usalama wa chakula na hata kupambana na magonjwa ya kuhara na kipindupindu.

Bahati mbaya ni kwamba, mamalishe wengi wanafanyia shughuli zao kwenye maeneo ambayo siyo rasmi, yasiyokuwa na huduma muhimu zikiwamo za vyoo na maji, hivyo suala la usafi linaweza kuwa na changamoto.

Kwa hali hiyo wanaweza kujikuta wakitoa huduma, ambazo haziko salama kwao na hata kwa wateja wao, hivyo uboreshaji wa maeneo ya shughuli zao ni muhimu, ili kuepuka kusababisha magonjwa.

Usafi wa mazingira ikiwamo matumizi ya vyoo pamoja na tabia ya usafi, hasa unawaji wa mikono kwa sabuni ni vya msingi kwao na jamii kwa ujumla na inaweza kuwa kinga, kuliko kufanya mambo kienyeji na kusababisha maradhi.

Hivyo vyombo na eneo la kutayarishia chakula halina budi kuwa safi na mbali, huku chakula kikihifadhiwa kwenye vyombo vilivyofunikwa kwa ajili ya kulinda afya za wateja

Kimsingi hayo ni baadhi ya mambo muhimu ambayo wataalamu wa afya wamekuwa wakisisitizia jamii kuyazingatia ingawa wapo watu, ambao wanadhani uchafu ni jambo la kawaida.

Wakati hali ikiwa hivyo kwa baadhi ya mamalishe, hata wanaochinja kuku kwenye masoko mbalimbali na hasa jijini Dar es Salaam, nao wanachangia uchafuzi wa mazingira na kuhatarisha afya za wengine.

Kwenye baadhi ya masoko yakiwamo ya Shekilango na Manzese, wanamwaga damu ya kuku iliyooza ikiwa imechanganywa na taka nyingine na kusababisha harufu kali mitaani.

Wapita njia na wale wanaokwenda kupata mahitaji kwenye masoko hayo watakuwa ni mashahidi wa kile ninachoeleza hapa kwani kwa namna moja ama nyingine watakuwa wameshakumbana na harufu hiyo.

Hayo yanafanyika wakati viongozi wa masoko wapo na wao wanafukizwa na harufu hiyo kali inayoumiza na inawezekana ikawa ina madhara ya kiafya kwao na hata kwa wanaofika kupata mahitaji.

Kwa hali kama hiyo, kuna umuhimu wa kuchukua hatua za kuandaa maeneo ya kumwaga damu hiyo na kuifikia kuliko kuicha ioze na kuanikiza harufu hiyo kali mitaani yenye kukera.

HABARI KITAIFA

# 280,000 wapata pasipoti mpya za kielektroniki

**Na Romana Mallya**

IKIWA imesalia siku moja ili serikali isitishe matumizi ya hati za zamani za kusafiria, idadi ya waliojitokeza kuomba hati mpya za kielektroniki tangu mchakato huo uanze ni 280,877.

Akizungumza na Nipashe jana jijini Dar es Salaam, Msemaji wa Idara ya Uhamiaji nchini, Ally Mtanda, alisema takwimu zinaonyesha tangu mchakato huo uanze Januari 31, mwaka 2018 hadi juzi idadi iliyojitokeza na kupata hati mpya ndiyo hiyo.

Wakati akizungumza hayo gazeti hili jana lilishuhudia idadi kubwa ya watu waliojitokeza kwenye ofisi ya uhamiaji iliyopo Kurasini wakisubiri kupatiwa huduma hiyo kabla ya siku ya mwisho inayoishia kesho.

Mtanda alisema idadi ya hati mpya ambazo zimetolewa kwa watu wa kawaida ili kuwasaidia wakati wanasafiri nje ni 281,544.

"Idadi ya hati za kusafiria za kiutumishi ambazo hupewa viongozi wa serikali waandamizi zilizotolewa hadi juzi ni 499, hati za kusafiria za kidiplomasia wakiwamo mabalozi wanaowakilisha Tanzania nchi mbalimbali zimetolewa 1,829 na hati za kusafiria maalum za kidiplomasia zinazotolewa kwa viongozi wakuu zimetolewa ni tano," alisema.

Mtanda alisema Uhamiaji itasitisha matumizi ya hati za kusafiria za zamani ifikapo kesho.

"Agizo la kusitisha hati za kusafiria za zamani bado lipo pale pale hivyo Watanzania wanaosafiri kuanzia Februari Mosi, hati hizo za kusafiria za zamani hazitatumika, tunaomba wasizitumie kwa sababu hawataweza kutoka nje ya nchi," alisema.

Alisema Watanzania ambao wapo nje ya nchi wenye hati za kusafiria za zamani bado wataweza kuingia nchini iwapo nchi wanazotoka zitawaruhusu kuendelea kutumia kuja Tanzania.

"Lakini wakitaka kutoka Tanzania kurudi nchi nyingine duniani hawatatoka na hizo za zamani, tulijiwekea miaka miwili ukomo wake unaoisha Januari 31," alisema.

Alisema malengo waliyojiwekea kama uhamiaji wameyafikia ya kuwawezesha watu kusafiri kwenda nje ya nchi.

"Hati za kusafiria za zamani kwa kipindi cha miaka 10 uhamiaji iliweza kuzitoa 950,000 kwa kasi tunayoenda nayo kwa miaka miwili kasoro tunaona tupo vizuri, hakuna Mtanzania ambaye amekosa kusafiri, " alisema.

Alisema wameweza kufungua dawati la hati za kusafiria za dharura kama wagonjwa, watumishi wa serikali, wafanyabiashara mwenye uthibitisho wa safari ya dharura wamekuwa wakihudumiwa ndani ya siku moja na kuzipata.

Alisema huduma zao zinatolewa katika vituo 31 nchi zima pamoja na kwenye balozi 44 ambako ipo mifumo imefungwa ya kuwasilishwa maombi kwa wale walio nje.

Mtanda alifafanua kuwa kinachositishwa kesho ni matumizi ya hati ya kusafiria ya zamani, lakini ubadilishaji utaendelea kadri zinavyoisha.

"Tutafunga matumizi ya hati za kusafiria siyo kubadilisha bila gharama yoyote, ada itakuwa ni ile ile. Zipo ofisini kwetu hati za kusafiria za zamani ambapo tangu apewe hawawahi kuja uhamiaji kuzichukua, zipo kama 2,000 idadi kamili mpaka niitafute," alisema.

Kuhusu malalamiko ya kuchelewa kutolewa hati hizo, Mtanda alisema kwa sababu vituo viwili vya Kurasini na Zanzibar vinapokea maombi ya hati za kusafiria ya nchi nzima, hata kama itachelewa haiwezi kupita wiki zilizowekwa.

Kuhusu foleni, alisema awali walikuwa wameongeza muda hadi saa nne usiku kutokana na idadi ya watu, lakini tangu mwaka huu uanze wamepungua na inapofika saa nane mchana huisha.

# Mapato Hospitali Sekou

**Na Mary Geofrey,** MWANZA

HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa wa Mwanza Sekou Toure, imeongeza mapato ya kila mwezi kutoka Sh. milioni 50 hadi 300 katika kipindi cha miaka minne.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Engelbert Rauya, aliyasema hayo jana jijini hapa, wakati akizungumza na waandishi wa habari na maofisa mawasiliano wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, katika ziara yake ya kampeni ya 'Tumeboresha Sekta ya Afya'.

Lengo la kampeni hiyo ni kuangazia mafanikio ya Serikali katika sekta ya afya nchini.

Dk. Rauya alisema sababu za mapato kupaa ni kutumia mfumo wa kieletroniki wa ukusanyaji mapato, kufunga kamera sehemu zote za hospitali zinazodhibiti watumishi kuingiza mapato mifukoni.

Alisema pia wanashirikiana na askari wa Suma JKT kuhakikisha kila mgonjwa anayetoka katika hospitali hiyo anakuwa na risiti za matibabu na kama hana hulazimika kwenda kuonyesha aliyempa huduma.

"Haya yamesaidia kwa kiasi kikubwa kudhibiti mapato ya hospitali, badala ya kuingia kwenye mifuko ya watumishi sasa yanaingia kwenye mfumo rasmi wa serikali na hivyo kumefanya yaongezeke hadi kufika Sh. milioni 300 kwa mwezi," alisema Dk. Rauya. Alisema kuwapo mfumo wa mzuri wa usimamizi wa mapato na ukaguzi wa matumizi na mapato ya hospitali hiyo kumesaidia kuwapo kwa makusanyo ya kutosha.

Alisema kwa kutumia mapato hayo wanafanya ukarabati wa jengo la dharura kwa gharama ya Sh. milioni 10 na kutenga asilimia 50 ya mapato kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba.

Alisema miongoni mwa dawa na vifaa tiba wanavyonunua ni vya kujifungulia hali inayofanya kupata huduma za uzazi bure.

Alisema pia wanatoa motisha kwa watumishi wanaofanya vizuri ili kuboresha utendaji kazi.

Naye Muuguzi Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Uyanjo Nkumbi, alisema idadi ya wajawazito wanaojifungua kwa mwezi imeongezeka kutoka 500 hadi 1,000 kwa mwezi.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

**ISO 9001:2015 CERTIFIED**

## TAHADHARI KWA UMMA

NDUGU WATANZANIA;

KAMA MNAVYOFAHAMU, LAINI ZA SIMU AMBAZO HAZIJASAJILIWA KWA KUTUMIA NAMBA YA KITAMBULISHO CHA TAIFA **(NIN)** NA KUTHIBITISHWA KWA ALAMA ZA VIDOLE ZILIANZA KUZIMWA TAREHE 20 JANUARI, 2020 USIKU NA **ZOEZI LINAENDELEA.**

**HAKIKI TENA USAJILI WA LAINI ZAKO KWA KUPIGA NAMBA *106# NA UCHUKUE HATUA STAHIKI SASA.**

1.0 KWA WALIOSITISHIWA HUDUMA ZA LAINI ZAO ZA SIMU KUANZIA TAREHE 20.01.2020 WANAWEZA PIA KUENDELEA NA UTARATIBU WA USAJILI KWA LENGO LA AMA KURUDISHA LAINI ZAO ZILIZOFUNGWA KAMA ZITAKUWA BADO ZIPO AU KUPATA LAINI MPYA. **ZOEZI HILI NI ENDELEVU.**

2.0 KWA WATUMIAJI/WAOMBAJI **(WATANZANIA)** WAPYA WA LAINI ZA SIMU WATAENDELEA KUSAJILIWA MUDA WOTE KWA KUTUMIA NAMBA YA KITAMBULISHO CHA TAIFA NA KUTHIBITISHA KWA ALAMA ZA VIDOLE. **HUDUMA HIYO NI ENDELEVU PIA.**

3.0 MATUMIZI SAHIHI YA VITAMBULISHO WAKATI WA USAJILI WA LAINI ZA SIMU(ZINAZOTUMIKA AMA KWA AJILI YA MAWASILIANO YA SIMU ZA SAUTI AU VIFAA VYA MAWASILIANO MENGINE)UKO KATIKA MAKUNDI YAFUATAYO: -

3.1 Sisi wa-**Tanzania** kitambulisho chetu ni kile cha Taifa kitolewacho na NIDA kwa vigezo vyao;

3.2 Kwa wageni wanaokaa hapa nchini **chini ya miezi sita** wanasajili laini za simu kwa kutumia namba za Hati zao za kusafiria na kuthibitisha kwa alama za vidole;

3.3 Kwa wageni wanaokaa **zaidi miezi sita** wanatumia vitambulisho ***(Legal Resident ID)*** ambavyo hupewa na NIDA (Hii ni kwa mujibu wa utaratibu wa idara ya Uhamiaji na NIDA);

3.4 Kwa wanadiplomasia wanatumia Hati zao za kusafiria pamoja na vitambulisho vyao vinavyotolewa na Wizara ya Mambo ya nje; na

3.5 Kwa wakimbizi wanatumia vitambulisho vyao ambavyo hutolewa na NIDA ***(Hii ni kwa mujibu wa utaratibu wa idara ya Uhamiaji na NIDA),***

4.0 KATIKA KUJIRIDHISHA KUWA WALIOSAJILI LAINI ZAO ZA SIMU WAMETUMIA VITAMBULISHO SAHIHI, TCRA KWA KUSHIRIKIANA NA WATOA HUDUMA ITAFANYA ZOEZI LA KUHAKIKI LAINI ZOTE ZITAKAZOKUWA ZIMESAJILIWA ILI KUWAONDOA WALE WALIOSAJILI LAINI ZAO AMA KWA KUTUMIA VITAMBULISHO VYA WATU WENGINE AU KWA KUTUMIA KITAMBULISHO TOFAUTI SAMBAMBA NA KUWACHUKULIA HATUA ZA KISHERIA.

5.0 IKUMBUKWE PIA KWAMBA KUSAJILI LAINI YA SIMU KWA KUTUMIA KITAMBULISHO CHA MTU MWINGINE NI KOSA SANJARI NA KUPEWA LAINI ILIYOSAJILIWA NA MTU MWINGINE.

6.0 **ONYO NA TAHADHARI ZINAENDELEA KUTOLEWA KWA MAKUNDI YOTE YALIYOORODHESHWA KWENYE KIPENGELE CHA 3.0 HAPO JUU, KUTOTUMIA KITAMBULISHO KISICHOKUHUSU WAKATI UNASAJILI LAINI ZAKO ZA SIMU** (ZINAZOTUMIKA AMA KWA AJILI YA MAWASILIANO YA SIMU ZA SAUTI AU VIFAA VYA MAWASILIANO MENGINE).

**Imetolewa na Mkurugenzi Mkuu**
**Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)**
**24 Januari, 2020**

215600102

# Wabadhirifu Stamico sasa wawashiwa taa nyekundu

**Na Frank Monyo**

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, ametoa siku saba kwa Mtendaji Mkuu wa Shirika la Madini la Taifa (Stamico), kuwashughulikia wale wote wanaoshirikiana kufanya ubadhirifu katika mradi wa kuchoronga miamba ya madini.

Agizo hilo alilitoa jana jijini Dar es Salaam wakati wa kufunga mkutano wa mwaka wa Baraza la Wafanyakazi wa Stamico, huku akimtaka Mtendaji Mkuu wa shirika hilo, Dk. Venance Mwasse, kuchukua hatua za haraka.

Alisema watu wamekuwa wakitengeneza stakabadhi na mihuri feki na kusababisha serikali kushindwa kufikia malengo yake, hivyo kwa yoyote atakayechukuliwa hatua katika mradi huo asimlaumu mtendaji mkuu wa Stamico bali amlaumu waziri kwani yeye ndiye aliyetoa maagizo hayo.

Aliongea kuwa Wizara ya Madini ilitoa mtambo wa kochoronga miamba ya madini wenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni mbili, na kwamba lengo likiwa ni kupata faida baada ya kufanya kazi hiyo katika migodi mbalimbali nchini, lakini kumekuwa na watu ambao sio waaminifu katika mradi huo.

“Nafurahi kwamba mpaka sasa mmefanya kazi ya Sh. bilioni 4 na kupata faida kidogo ya Sh. milioni 600 ...mimi imani yangu na taarifa nilizonazo mngepata zaidi ya milioni 600, lakini ninazo taarifa katika mradi wa uchorongaji kuna mikono isiyo misafi inayohujumu mradi huo,” alisema Biteko na kuongeza kuwa: “Tumewapa mtambo hapa wa kuchoronga tumenunua kwa fedha nyingi ambazo tungeweza kununulia dawa kwenye hospitali na zingejenga madarasa.”

Alisisitiza kuwa wale wote wanaojijua wanafanya ujanja ujanja katika mradi huo wajiandae kuchukulia hatua, kwani wapo Watanzania wengi ambao wanaweza kusimamia mradi huo na serikali ikapata faida. Biteko aliitaka Stamico kuwa makini na mikataba yote ambayo wanaingia kwani inapaswa kupitishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Canara Bank (Tanzania) Ltd.

(Together we can build a better life)

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2019 *(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo Mwaka ya sasa 31 Desemba 2019 | Robo Mwaka uliopita 30 Septemba 2019 |
|---|---|---|
| **A MALI** | | |
| 1 Fedha Taslimu | 405.33 | 451.67 |
| 2 Salio katika Benki kuu ya Tanzania | 6,601.37 | 8,437.49 |
| 3 Uwekezaji katika Amana za serikali | 25,372.07 | 29,524.24 |
| 4 Salio katika Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 668.77 | 258.50 |
| 5 Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 67.32 | 84.85 |
| 6 Miamala Baina ya Matawi | 0.00 | 0.00 |
| 7 Bili zilizoafikiwa | 0.00 | 0.00 |
| 8 Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0.00 | 0.00 |
| 9 Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 36,885.00 | 26,170.00 |
| 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0.00 | 0.00 |
| 11 Mikopo Halisi Iliyopo | 35,482.73 | 37,459.06 |
| 12 Mali Nyingine | 873.34 | 971.65 |
| 13 Uwekezaji wa Hisa | 0.00 | 0.00 |
| 14 Akaunti za udhamini | 0.00 | 0.00 |
| 15 Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 722.76 | 785.76 |
| **16 JUMLA YA MALI** | **107,078.69** | **104,143.22** |
| **B DHIMA** | | |
| 17 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 32,500.00 | 26,750.00 |
| 18 Amana za Wateja | 37,399.46 | 40,912.39 |
| 19 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0.00 | 0.00 |
| 20 Amana Maalumu | 0.00 | 0.00 |
| 21 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0.00 | 0.00 |
| 22 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 0.00 | 0.00 |
| 23 Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,215.40 | 1,133.45 |
| 24 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0.00 | 0.00 |
| 25 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0.00 | 0.00 |
| 26 Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 0.00 | 0.00 |
| 27 Dhima Nyingine | 28.66 | 15.10 |
| 28 Madeni | 0.00 | 0.00 |
| **29 JUMLA YA DHIMA** | **71,143.52** | **68,810.94** |
| **30 MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29* | **35,935.17** | **35,332.28** |
| **C FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 32,830.00 | 32,830.00 |
| 32 Akiba ya Mtaji | 1,117.25 | 479.44 |
| 33 Mapato Yaliyobakizwa | 535.62 | 535.62 |
| 34 Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1,452.29 | 849.41 |
Sasa, utaratibu uliowekwa hapo muda wa kumuona mgonjwa ni saa 12 asubuhi hadi saa 1.00 asubuhi na mchana saa 6.00 anaruhusiwa kuingia ndugu mmoja tu mwenye chakula, huku ikisisitizwa “hospitali yenyewe pia inatoa vyakula kwa wagonjwa.”

Muda wa jioni, kuona mgonjwa ni kuanzia saa 10.00 jioni hadi saa 12.00 jioni. Hapo ndugu wote wanapaswa kuondoka, hivyo wagonjwa wanabaki na matabibu na timu ya wahudumu hospitalini.

Ni utaratibu unaoweza kuonekana mzuri kwa namna fulani, lakini upande mwingine una sura ya matatizo, hususan kwa wagonjwa, ikiwamo kukosa huduma muhimu na ya lazima kwa baadhi yao kama vile kulishwa vyakula na kubadilishwa nguo.

Katika taarifa yake, Mkurugenzi hakutaja idadi ya manesi waliopo hospitalini. Hapo narejea kiulizo fulani, je, idadi hiyo inalingana na uhalisia wa majukumu yao?

Nasema hivyo, maana wahudumu hao wa afya ndio wenye jukumu la kuwahudumia wagonjwa, kulingana na hali walizo nazo.

Wagonjwa wengi naamini wanapewa dawa vizuri, lakini mlo wao usiwe unajitosheleza. Hapo, narejea kwa nilichoshuhudia kwa mgonjwa na wenzake wodini ambao hawakuwa na hali nzuri zaidi.

Tunaelimishwa ‘chakula ni dawa.’ Baadhi kutokana na uhalisia wa hali zao, hawali au hawalishwi inavyotakiwa, wanateseka kwa njaa, msingi wa hoja nauona hata manesi wanashindwa kujigawa kwa kuelemewa majukumu na aina ya wagonjwa walio nao.

“Afadhali tusaidie, mgonjwa wako mbishi sana kula, tusaidieni. Tunaelemewa... wa aina hii wako wengi,” anatamka mkunga mmoja, kueleza uhalisia wake.

Hospitalini Mloganzila, kuna wahudumu wanaogawa vyakula, ingawaje Nipashe ilishuhudia ugawaji uko katika mfumo unaofanana na ‘shule’ kwa maana hauangalii mahitaji maaluma ya mgonjwa husika.

Mgonjwa wangu, alihitaji vitu laini, lakini aliletewa makande. Ina maana bahati ya kuwa na huduma ‘Plan B’ ndiyo ilimnusuru kiafya.

Kazi ya kusamba vyakula hivyo, inafanywa na wahudumu maalum wanaoweka mabakuli ya vyakula kwenye meza za wagonjwa katika mfumo mmoja.

Ni wazi katika, uhalisia manesi ambao ndio wahudumu wakuu wanaelemewa na mazingira ya kazi, ikiwamo jukumu la kulisha, inawezekana wapo katika mazingira hayo kubaki na njaa, kama ilivyokuwa kwa mgonjwa wangu.

Nipashe ilishuhudia uji na mtori unavyoachwa saa 12 jioni, ndivyo unavyokutwa asubuhi inayofuata. Ni eneo ambalo hospitali uongozi unapaswa kuliangalia katika mipango mkakati yake ya kiutendaji, kwa maboresho.

Mbadala unaweza kuwekwa hata kwa maboresho ya kuruhusu ndugu walau mmoja kuingizwa wodini muda fulani, pale mahitaji maalum yanapotokea.

Ni njia moja kumtua nesi mzigo mzito na wakati huo huo, kuijengea picha nzuri ya kazi safi inayofanyika Mloganzila- Muhimbili.

**IDADI YA VIFO**

Mkurugenzi Profesa Museru katika taarifa yake anabainisha kuwa huo idadi ya vifo imekuwa ikipungua kutoka asilimia 14.9 iliyokuwepo katika kipindi cha robo mwaka cha Julai hadi Septemba, 2018 na kufikia asilimia 10.4 katika kipindi cha Julai-Septemba mwaka jana.

Anaeleza, takwimu za Muhimbili MNH Upanga) zinaonyesha katika kipindi cha robo mwaka cha Julai hadi Septemba 2018, wagonjwa waliolazwa walikuwa ni 12,375 na kulitokea vifo 1,000 ambayo ni asilimia 8.1.

“Vilevile katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2019 MNH Upanga ililaza wagonjwa 17,230 na kati ya hao vifo vilikua 1,673 ambayo ni asilimia 9.7,”anasema.

Hivyo basi, takwimu kati ya MNH-Mloganzila na MNH-Upanga za asilimia ya wagonjwa waliofariki hazitofautiani sana, MNH-Upanga ni asilimia 9.7 wakati MNH-Mloganzila ni asilimia 10.4 katika robo ya Julai - Septemba, 2019.

“Hatua hii inaonyesha juhudi ambazo zinafanyika za kuboresha utoaji wa huduma katika MNH-Mloganzila zinazaa matunda,” anasema Profesa Museru,

**IDADI MADAKTARI**

Kuhusu hali ya madaktari, Profesa Museru ana maelezo: “Tungependa kufafanua kwamba, Hospitali ya MNH-Mloganzila ina madaktari bingwa 52, madaktari wa kawaida 50 na kwa sasa ina madaktari tarajali 53.”

Anasema, licha ya madaktari hao bingwa walioajiriwa MNH-Mloganzila kutoa huduma, pia wanashirikiana na madaktari bingwa kutoka MNH-Upanga katika kutoa huduma hapo MNH- Mloganzila.

“Vilevile hospitali hii ina madaktari wawili waliobobea wenye hadhi ya Profesa kutoka Korea nao wapo wanatoa huduma,” anasema katika taarifa yake hiyo, akikanusha dai la madaktari waliopo mafunzoni wanafanya kazi bila usimamizi.

Kwa mujibu wa mkurugenzi, hospitali imejiwekea utaratibu wa kila mgonjwa anayefika kupata huduma, anaonwa na daktari bingwa kwa ajili ya kufanyiwa uamuzi.

“Tangu MNH ipewe dhamana ya kusimamia hospitali hii, tumejielekeza katika kutatua changamoto zilizokuwapo katika utoaji huduma na kwa kiasi kikubwa imeonyesha mafanikio ambayo yanaonyesha kuongezeka idadi ya wagonjwa, pia kuna ushuhuda wagonjwa waliotibiwa na kuridhika na huduma zetu,” anasema.

Nipashe katika eneo hilo, inakiri kushuhudia madaktari wanafunzi walioendesha matibabu katika umakini unaoleta faraja kwa mgonjwa na wanandugu.

Mtazamo tu ni kwamba madaktari wanafunzi wanapita kila mara vitandani mwa wagonjwa, wanapaswa kupewa moyo na siyo kuwakatisha tamaa kwa manung’uniko dhidi yao, ikizingatiwa ndio madaktari wa kesho.

***Makala hii inachangiwa na uzoefu wa kuwapo hospitalini Mloganzila kwa wastani zaidi ya wiki, ikianzia Muhimbili - Upanga, pia taarifa rasmi ya hospitali mwezi huu.*** .

> **Vilevile katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2019 MNH Upanga ililaza wagonjwa 17,230 na kati ya hao vifo vilikua 1,673 ambayo ni asilimia 9.7.**



Sehemu ya wodini Mloganzila.

> **Hatua hii inaonyesha juhudi ambazo zinafanyika za kuboresha utoaji wa huduma katika MNH- Mloganzila zinazaa matunda.**

# Asilimia 74 Watanzania wanajifungua hospitalini



Kinamama wa Arusha wakipata huduma za kliniki ya wazazi. **PICHA: MTANDAO**

Na Yasmine Protace

WAJAWAZITO wanapohudhuria kliniki, ni hatua inayosaidia kuwawezesha kujifungua kwa usalama zaidi, huku ikiwa zimemsaidia daktari kuelewa kitu gani kifanyika wakati wa kujifungua.

Pia, kwa mama mjamzito kutokana na kubaini tatizo pale anapokuwa amahudhuria kliniki, kuna mambo anajifunza yanayokuwa mkombozi katika kuilea mimba mpaka wakati wa kujifungua.

Inapotokea mjamzito hatashiriki kliniki katika kipindi cha ujauzito mwanzo hadi kujifungua, anakuwa katika hatari ya kupata tatizo kutokana na ujauzito wake, hasa wakati wa kujifungua katika sehemu isiyofaa.

Hivyo, ni hali inayotoa umuhimu wa wajawazito kuhudhuria kliniki ikiwa ni jambo jema linalosaidia kufanikisha mzazi anapopata elimu bora ya uzazi, itamsaidia kipindi cha ujauzito na baada ya kujifungua.

Kukosa uelewa hususan mahudhuri ya kliniki, ni hali inayochangia kwa baadhi ya wajawazito kutojifungua salama, huku wengine wakipata shida ya uzazi kutokana na kukosa kuhudhulia kliniki.

Ili kuhakikisha afya ya mama na mtoto inakuwa salama, serikali imekuwa ikiwahamasisha wajawazito kuhudhuria kliniki kipindi cha mwanzo wa ujauzito, lengo ni kuwasaidia kujifungua salama katika vituo vya afya.

Hivyo, kuhudhuria kliniki kwa wajawazito kunasaidia idadi yao kubwa kujifungua katika vituo vya afya na zahanati.

Inahimizwa, kama inatokea wajawazito hawatakuwa na elimu kamili muhimu ya kuhudhuria kliniki, ni hali inayoweza kuchangia wajawazito kujifungua katika maeneo yasiyo salama kwa afya ya mama na mtoto.

Iinaeleweka kwamba, wajawazito wanapohudhuria kliniki wananufaika na elimu ya usalama wa kutunza mimba, faida za matumizi sahihi ya dawa kuendena na hali waliyonayo.

Kumekuwapo ushuhuda wa namna nyingi, wajawazito wasiohudhuria kliniki wanapata changamoto kukosa damu nyingi, kifafa cha mimba na kujifungua watoto wenye kilo ndogo.

Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, anasema kuwa asilimia 74 ya wajawazito wamejifungulia kwenye vituo vya kutoa huduma za afya nchini.

Kupitia taarifa yake ya utekelezaji kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya huduma na maendeleo ya jamii wa wizara kwa kipindi cha Julai hadi Desemba mwaka jana, , Waziri Ummy anasema:

“Katika kipindi hiki matarajio yalikua ni wajawazito 1,100,000 wangejifungua,hata hivyo takwimu zinaonesha kuwa jumla ya wajawazito 813,923 sawa na asilimia 74 walijifungua kwenye vituo vya kutoa huduma,”

Anaongeza kuwa wajawazito waliofanya mahudhurio ya kliniki, waziri huyo anasema jumla ya wajawazito 797,803 sawa na asilimia 73 ya walengwa, walifanya mahudhurio ya kliniki kama mwongozo ulivyoelekeza.

Waziri Ummy, anafafanua asilimia 87.4 ya wajawazito sawa na kinamama 886,810 walipatiwa dawa za kujikinga na malaria na jumla ya dozi 2,844,174 sawa na asilimia 84.6 walipewa dawa ya kuzuia upungufu damu.

Kwa mujibu wa Waziri Ummy, wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, ilihakikisha dawa muhimu za kuzuia na kutibu kifafa cha mimba, kukinga na tiba ya upotezaji damu baada ya kujifungua.

Hatua ya kutibu watoto chini ya miaka mitano, nayo ili iliimarika kwa zaidi ya asilimia 85.

Moja ya mambo yanayohimizwa kupitia Mpago wa Maendeleo ya Afya (MMAM) yenye miaka zaidi ya 12 sasa tangu kuanza kutimzwa, inahimiza katika kulinda afya za wajawazito, wazazi na watoto wao.



Mashabiki waliotekwa na mechi uwanjani. **PICHA: MTANDAO.**

## Mashabiki soka waongoza msongo, shinikizo

**LONDON,** Uingereza

WATAFITI kutoka Chuo Kikuu cha Oxford nchini hapa wamebaini mashabiki wa soka wanaongoza katika msongo wa mawazo, kutokana na upenzi wao uliopitiliza wawapo uwanjani kushuhudia mechi.

Ni hali ambayo wataalamu hao watafiti wanasema, inawaweka katika hatari zaidi ya kupatwa na maradhi ya shinikizo la damu

Uzoefu uliochukuliwa kutoka na ushabiki katika mashindano ya kombe la dunia mwaka 2014, vipimo vya mate vilionyesha hatari hiyo, tena kwa viwango vinavyofanana wake kwa waume.

Mtafiti Dk. Martha Newson, anasena mashabiki waliojikita zaidi kupendelea timu moja, wako katika hatari zaidi kuopatwa na shikinizo wakati wanashuhudia mechi inayoendelea.

Anaongeza: "Wale mashabiki wa kawaida, nao hawako salama, ingawaje si vibaya sana."

Kwa mujibu wa watafiti, huko nyuma hatari ya shinikizo la damu na athari zake, ilikuwa zaidi katika mechi kubwa. Lakini sasa katika mechi zote na mashabiki wa aina zote.

Mtaalamu mwingine, anasema mashabiki ambao wanaumizwa na timu zao kufanya vibaya, wengi wamekuwa wakijipooza kihisia kwa kutumia matendo kama kukumbatiana kupunguza makali ya maumivu.

AFYA

# Taasisi ya lishe katika mageuzi kumwondolea mtoto utapiamlo

• Kiwango afya duni kushushwa • Wazazi nao kuangukia afya njema • Ubia na wazalishaji mafuta kula



Watoto waliopo katika hatua za makuzi, ambao lishe bora ni sehemu ya hitaji muhimu. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Mary Geofrey**

SERIKALI imeanzisha mpango mkakati wa kuhakikisha kila mtoto chini ya miaka mitano, anapata virutubisho vya kupunguza udumavu wao wenye umri huo.

Ni mikakati iliyowekwa kuongeza virutubisho kwenye mafuta ya kula na chakula kama unga wa ngano, wakati vikitengenezwa kiwandani.

Mpango mwingine inataja ni wa kushirikiana na wadau wa kilimo, kuhamasisha ulimaji na utumiaji mazao iliyoongezwa virutubishi kama viazi lishe na mahindi lishe vyenye kiwango kikubwa cha Vitamin A na maharage yenye vitamini, madini chuma na zinki.

Mkakati huo, unasimamiwa na kutekelezwa na Taasisi ya Chakula la Lishe (TFNC), kwa lengo la kupunguza udumavu kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano

> **Japo tumefanikiwa kupunguza kiwango cha udumavu, lakini kiwango cha asilimia 32 ni malengo ya nchi na Shirika la Afya Duniani (WHO).**

kutoka asilimia 32 zilizopo sasa hadi kufika chini ya asilimia 20.

Aidha, inalenga kupunguza utapiamlo kutoka asilimia 3.5 za sasa hadi chini ya hapo na kupunguza tatizo la upungufu wa damu, kwa wajawazito kutoka asilimia 29 hadi kumalizika.

**MKURUGENZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa TFNC, Dk. Germana Leyna, ametoa ufafanuzi huo, ukiwa ni sehemu ya mafanikio ya taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kuelezea mafanikio katika kampeni iitwayo 'Tumeboresha Sekta ya Afya'.

Lengo la kampeni hiyo ni kuangazia miaka minne ya Serikali na mafanikio yaliyopatikana katika sekta za afya nchini.

Dk. Leyna anasema, "Kwa kushirikiana na sekta ya binafsi tumetekeleza kanuni za kuongeza virutubisho kwenye chakula. Lengo letu ni kuhakikisha tunamaliza tatizo la udumavu utapiamlo kwa watoto chini ya miaka mitano,"

Anasema, kwa sasa wanaongeza virutubisho vya Vitamin A kwenye mafuta ya kula, Vitamin B 12, zinki, tindikali aina ya foliki na madini chuma kwenye unga wa ngano na mahindi.

Dk. Leyna anasema, pia wanashirikiana na wadau mbalimbali wakiwamo wazalishaji wadogo wa chumvi na viwanda vya kuzalisha bidhaa zinazoongezewa madini.

"Japo tumefanikiwa kupunguza kiwango cha udumavu, lakini kiwango cha asilimia 32 ni malengo ya nchi na Shirika la Afya Duniani (WHO)," anasema Dk. Leyna.

Anataja kufanikiwa kupunguza aina nyingine za utapiamlo na watoto chini ya miaka mitano wanakonda, kuwa na uzito chini ya kiwango wanachostahili, kutoka asilimia 4.5 mwaka 2015/16 hadi asilimia 3.5 mwaka juzi.

Dk. Leyna anasema upungufu wa damu kwa wanawake walio katika umri wa kuzaa, kwa maana ya kati ya miaka 15 hadi 49 , nao unapunguzwa kutoka asilimia 45 katika kipindi kilichotajwa.

Eneo lingine, kuongeza idadi ya watoto wanaolishwa vizuri na wanaonyosheshwa maziwa ya mama pekee kwa kipindi cha miezi sita ya mwanzo wa uhai wao, kutoka asilimia 41 zan mwaka 2014 hadi asilimia 58 mwaka juzi.

Pia, watoto wenye umri chini ya miaka mitano, wamefanikishwa kulishwa kama inavyotakiwa, kwa idadi na makundi ya vyakula kutoka asilimia 20 hadi 30 kwa kipindi hicho.

"Kwa kufanya hivi tumetelekeza mikakati ya kisekta ya kitaifa ya Wizara ya Afya," anasema Dk. Leyna.

**MAFANIKIO YALIYOPO**

Mkurugenzi huyo anasema, katika kipindi cha miaka minne sasa, wameanzisha mpango jumuishi wa lishe kitaifa, ambao ni wa miaka mitano, kuanzia Julai 2016 hadi hadi Juni mwaka ujao.

Anasema ni mpango ambao serikali imefanikiwa kuunganisha nguvu za wadau wa sekta mbalimbali katika utekelezaji wa afya lishe, kwa sababu shughuli zilikuwa zinaratibiwa na kufanywa na sekta ya afya pekee yake, kupitia Mpango wa Taifa wa Lishe.

Dk. Leyna anasema, baada ya kufanyika tathimini, ilibainika sekta ya afya inachangia asilimia 20 katika kukabiliana na tatizo ya lishe, wakati sekta nyinginezo zinachangia asilimia 80.

Anasema, mpango huo pia umesaidia kuongoza utekelezaji wa afya za lishe kutoka kila sekta, kama vile elimu, biashara, viwanda, kilimo, mifugo na fedha na anaongeza kuwa ufanisi wa utekelezaji uko katika Wizara ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi).

Dk. Lyena anaeleza kuwa, mafanikio mengine yaliyopata ni kupendekeza na kuhamasisha ongezeko la bajeti ya lishe katika halmashauri kutenga bajeti ya Sh.1, 000 kwa kila mtoto mwenye umri

AFYA

# Taasisi ya lishe katika mageuzi kumwondolea mtoto utapiamlo

chini ya miaka mitano, kwa ajili ya kutekeleza afua za lishe katika maeneo yao.

Kwa mujibu wa Dk. Lyena, awali halmashauri zilitenga bajeti ya Sh. 500 kila siku, lakini kuanzia mwaka 2018 bajeti iliongezwa hadi kufikia Sh. 1,000, ambayo ni takribani Sh. bilioni 11 kwa nchi nzima.

Anasema, wanaongeza madini joto kwenye chumvi katika utaratibu maalum wa kushirikiana na wamiliki wa viwanda vikubwa nchini, wakitekeleza mpango huo wakati wa kuandaa bidhaa zao.

Lingine analolitaja ni kuboreshwa utoaji elimu ya lishe kwa walengwa kiitwacho 'mkoba wa siku 1,000' unaojiendesha kuchangisha fedha za utengenezaji mikoba ya kupeleka elimu kuhusu umuhimu wa lishe bora kwa mtoto, kuanzia umri wa tumboni kwa mama hadi anapozaliwa na kuendelea kufikisha umri wa miaka miwili.

"Mkoba huu ni muhimu, kwa sababu kipindi hiki ni muhimu mtoto kupata mahitaji yote ya lishe, ikijumuisha virutubushi, ili kuboresha ukuaji wake kimwili na kiakili," anasema Dk. Leyna.

Anasema mkoba huo wenye maelezo na ufafanuzi bayana, unatumika kufundishia wajawazito na wawanake wenye watoto, kuhusu namna bora ya kuitunza mimba na mtoto mchanga, aina ya vyakula vya kumpa, katika kutafuta afya njema.

Dk. Leyna anasema, utafiti walioufanya unaonyesha mtoto anapokosa lishe au virutubishi katika umri huo, anapata athari za kudumu mwilini na kiakili, ambazo hazirekebishiki maishani mwake.

Anataja athari nyingine ni uwezekano wa mtoto kupata magonjwa wasiyo ya kuambukiza kirahisi, pindi anapofikia umri wa utu uzima. Dk. Leyna anasema mkoba huo wa siku 1,000 unahamasisha mabadiliko ya tabia katika kaya, ili zichukue hatua za kuboresha matunzo ya watoto tangu anapokuwa tumboni kwa mama yake, anazaliwa na kufikisha umri wa miaka miwili.

"TFNC inausambaza mkoba wa siku 100 katika mikoa yote nchini, kwa kushirikiana na wadau wa lishe," anasema Dk. Leyna.

Kadhalika anasema, wamefanikiwa kuandaa mkutano wa wadau wa lishe kila mwaka, kufanya tathimini ya utekelezaji wa mpango wa lishe jumuishi wa lishe kwa taifa. Mkutano huo unaleta hamasa na uelewa wa pamoja na vipaumbele vya nchi katika kupambana na utapiamlo nchini.

Anasema, wameendelea kusimamia utekelezaji wa Programu ya Mwezi wa Afya na Lishe ya Mtoto (CHNM), kwa kufanya maboresho ya kuongeza kipengele cha ufuatiliaji maendeleo ya mtoto katika vituo vya kutoa huduma za afya, pamoja kutoa nasaha za lishe.



Baadhi ya mahitaji muhimu katika lishe ya mtoto.

> **Baada ya kufanyika tathmini, ilibainika sekta ya afya inachangia asilimia 20 katika kukabiliana na tatizo ya lishe, wakati sekta nyinginezo zinachangia asilimia 80.**



Mafuta ya kula, ambayo sasa yanafayiwa mpango toka kiwandani kuwa na virutubisho.



Mtoto akiilishwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

### MTAZAMO WHO

Kuhusu hatua iliyopigwa, hadi sasa wamefanikiwa kuongeza viashiria vya ufuatiliaji namna ya kuaji na maendeleo ya watoto, kulingana na mapendekezo ya Shirika la Afya Duniani (WHO).

Mkurugenzi huyo anaeleza maboresho hayo ni muhimu, kwa sababu tatizo la utapiamlo linaathiri afya ya ukuaji watoto, na mkurugenzi anatoa ufafanuzi: "Maboresho haya yamewekwa katika kitabu cha afya ya mtoto, ambacho kimesambazwa katika mikoa 12 nchini."

Anataja mikoa hiyo ni Mwanza, Mara, Kigoma, Kagera, Geita, Shinyanga, Simiyu, Mbeya, Iringa, Njombe Songwe na Lindi na katika awamu ya kwanza wanatarajia kuendelea kusambaza katika mikoa mingine nchini.

Mafanikio mengine waliyopata, anayataja ni kuboresha maabara ya sayansi ya chakula, kwa kufanya ukarabati mkubwa, kuboresha vifaa kama vinavyiohusika kupima vyakula vinavyoongezwa virutubishi kiwandani na kibaiolojia na kipimo cha 'asidi ya foliki' ambayo ni njia ya 'maikrobiolojia.'

Vingine vinavyofanyiwa maboresho ni vifaa vya kupima wingi wa mafuta mwili kuthibitisha kiwango cha unyonyeshaji watoto wachanga kwa kutumia njia za kiatomiki.

Dk. Leyna anasema, vifaa hivyo zimegharimu zaidi ya Sh. milioni 990 kupitia ufadhili wa wadau wa maendeleo, likiwamo shirika la kimataifa la Gain Unicef na Taasisi ya Kimataifa ya Nguvu ya Atomiki.

Anasema ni maboresho yaliyoiewezesha taasisi kutoa huduma ya maabara kwa usahihi zaidi na kutathimini sampuli nyingi nyimgi kutoka ndani na nje ya nchi.

AFYA

# Kukosekana nguvu za kiume mjadala ‘tata’ ndani serikali

• Suzan Lyimo: Baba bandia... • Dk. Ndugulile: Miaka 50 ijayo...

**Na Sabato Kasika**

HADI sasa kuna mjadala wa kina unaoendelea kuhusu upungufu wa nguvu za kiume kwa baadhi ya watu na wanaoguswa zaidi, ni wenye umri kuanzia miaka 30 na kuendelea.

Ni kada inayotajwa kuongoza kwa kutumia dawa za kuongeza nguvu za kiume, kwa mujibu wa ripoti ya utafiti iliyotolewa mwaka 2015 na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), ikibainisha kuwa tatizo hilo linawakumba vijana wengi, hasa barani Afrika.

Ili kukabili shida hiyo, vijana wamekuwa wakitafuta dawa za kuongeza nguvu za kiume, pia kupunguza ukubwa wa adha ya namna hiyo, wateja wakubwa ni vijana wenye umri wa miaka 30 na kuendelea.

Aliyekuwa Mkurugenzi wa NIMR, Dk. Mwele Malecela, alianika hayo, walipogunduliwa aina dawa ya Mundex na anasema kada ya vijana na waathirika weengine wa kasoro hiyo ya kimwili, wamekuwa wakitumia mbinu mbalimbali, ili kuweka mambo sawa.

**MBADALA ULIOPO**

Kwa sasa baadhi ya watu wamekuwa wakitumia vyakula mbalimbali, wanavyoamini vina nafasi ya kwamba kwa namna moja ama nyingine vinaweza kusaidia kuwarejeshea nguvu hizo.

Imekuwa jambo la kawaida kukuta watu wanakunywa mchuzi wa samaki pweza, kutafuna vipande vya mihogo, nazi na karanga, ikiwa ni kuhakikisha wanaondokana na tatizo hilo, ambalo kila kukicha limekuwa mjadala.

Wakati juhudi hizo zikifanyika, waganga wa jadi nao hawako nyuma, kwani kwenye mabango yanayoelezea huduma zao wanazozitoa, huku dawa ya kwanza ikiwa ni kuongeza nguvu za kiume.

Kutokana na matangazo hayo ya waganga, baadhi ya watu huwafuata ili kupata huduma, ingawa haijulikani kama dawa hizo zinaweza kuwasaidia kuondokana na tatizo hilo.

**MBUNGE AFUNGUKA**

Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Suzan Lyimo, anaishauri serikali itoe elimu inayohusu wanaume kutokuwa na mbegu za kiume zenye nguvu tosha kwa ajili, ili kunusuru ndoa za Watanzania.

Mbunge huyo alifikisha tatizo hilo kwenye Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii Januari hii, wakati ikipokea taarifa ya utekelezaji wa shughuli zake jijini Dodoma.

Suzan, ambaye pia ni Waziri Kivuli wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, anasema ndoa nyingi zinavunjika, kwa watu kutopata watoto, kisa kikuu ni wanaume wanapokosa mbegu zenye uwezo kutengeneza mtoto.

Anasema sababu ta kuwapo mfumo dume, jamii ikiamini kwamba mwanamke ndiye mwenye tatizo, lakini hivi sasa imekuwa bayana, tatizo likionekana zaidi kwa wanaume.

“Kwa kweli ndoa nyingi sana zinavunjika. Ndoa hizi zinavunjika, kwa sababu ya watu kutopata watoto. Tatizo hili lilikuwapo, lakini linazidi kuongezeka,” anasema Lyimo.

Anasema, suala la ukosefu wa nguvu za kiume, linagusa uwezo wa mwanamume kumpa mwanamke ujauzito na kwamba hilo ni kubwa, hivyo ipo haja kwa serikali kutoa elimu sahihi ambayo inaifikia jamii kwa kina.

“Pia,ni vyema kutambua kwamba suala la nguvu za kiume zinazotafutwa, halina uhusiano wa kuweza kutengeneza mtoto. Mtu anaweza kuwa na nguvu za kiume na asiwe na uwezo wa kuzalisha,” anasema.

Suzan anaeleza umuhimu wa wanaume sasa wakubali kwa hiyari kwamba, kwa sababu wana tatizo na kwamba kuna haja ya kutolewa elimu, ili kutambua mzizi wa tatizo hilo, ili ichukuliwe hatua za kupata ufumbuzi sahihi na huenda ukawa wa kudumu, ikiwezekana.

**BABA BANDIA**

Mbunge huyo anasema katika mazingira hayo, yanahatarisha maisha ya ndoa, kuwapo idadi kubwa ya kinamama wenye watoto chini ya baba bandia.

“Kuna haja ya kutoa elimu ili tunusuru ndoa hizi, kwa sababu mimi kama mshauri, naletewa matatizo makubwa zaidi na wanawake wanafanya hivyo wakiogopa kupewa talaka,” anasema.



Mbunge Suzan Lyimo. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

> **Kuna haja ya kutoa elimu ili tunusuru ndoa hizi, kwa sababu mimi kama mshauri, naletewa matatizo makubwa zaidi na wanawake wanafanya hivyo wakiogopa kupewa talaka.**



Naibu Waziri, Dk. Faustine Ndugulile.

**WAZIRI NDUGULILE**

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndungulile, anasema changamoto ni kubwa na kwamba Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), imeanza maandalizi ya kutoa huduma ya ugumba.

Dk. Ndugulile, katika ufafanuzi wake hoja ya mbunge huyo, anasema utafiti duniani unaonyesha kuwa kwa miaka 50 kumekuwa na punguzo la asilimia 50 ya nguvu za kiume.

“Nilikuwa ninasoma utafiti mmoja, unasema katika miaka 50 ijayo basi wanaume wote hapa tutakuwa hamna kitu,” anasema Dk. Ndugulile.

Naibu Waziri huyo, anataja visababishi ni pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa, aina ya maisha na vyakula, hivyo kuna umuhimu wa kuzingatia lishe bora, ili kujinusuru na hatari hiyo.

Hata hivyo, anapinga hoja ya kuwepo watoto wengi ni wa ‘kubambikiwa baba’ kwa sababu wanaoenda kwa Mkemia Mkuu wa Serikali, ni wale wenye hofu vya kuwa watoto si wao.



# Wananchi wavamia mapori ya akiba

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

MAPORI ya akiba yanayomilikiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyama pori Tanzania (TAWA) mikoa ya Songwe, Singida na Mbeya yapo hatarini kutoweka kutokana na kuvamiwa na wananchi wanaojihusisha na ufyekajі wa miti, kilimo na ufugaji.

Pia mapori hayo yanakabiliwa na changamoto ya ujangili unaofanywa na wanavijiji wanaoishi karibu na mapori hayo ikiwamo uwindaji wa wanyama, uvuvi haramu na wizi wa nyara za serikali kama vile upasuaji wa mbao na uchimbaji wa dhahabu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jana, mameneja wa mapori hayo ya akiba ya Rukwati-piti na Rungwa, Kizigo na Mhasi walisema kuwa shughuli za kibinadamu zinaathiri mapori hayo kutokana na wananchi kutokutii sheria.

Meneja wa Pori la akiba la Rungwa-Kizigo na Mhasi, Patrick Kutondolana, alisema kuna tatizo la wananchi kutozingatia sheria ya kuishi umbali wa mita 500 kutoka eneo la pori la akiba na hivyo kuathiri shughuli za uhifadhi ndani ya mapori hayo, licha ya hatua mbalimbali za kisheria kuchukuliwa.

Alisema katika eneo la pori la akiba analolisimamia kuna vijiji zaidi ya 34 ambavyo vimezunguka mapori hayo ya akiba na kuwa wengi wa baadhi ya wananchi wamekuwa wakijihusisha na ujangili, uchimbaji holela wa dhahabu na uwindaji.

Kutondolana alipongeza jitihada za serikali kwa kudhibiti ujangili wa tembo ambao umepungua kwa kiasi kikubwa katika pori hilo na kwamba ujangili uliopo ni ule mdogo hususani nyakati za masika, ingawa wamekuwa wakifanya jitihada za kukabiliana nao.

Meneja wa Pori la Akiba la Rukwati-Piti, Jembe Chifuno, alisema hali ya ujangili katika pori hilo siyo mkubwa sana ingawa kumekuwa na ujangili wa wanyama wadogo wakiwamo nyati na uvuvi haramu wa samaki katika Ziwa Rukwa hususani nyakati za masika.

"Tumejipanga kuhakikisha tunakomesha ujangili wa wanyama na nyara za serikali zilizopo ndani ya mapori hayo, ndiyo maana katika msako wetu tunatumia vikosi maalum vya askari na msako wa majangili kwa kutumia ndege angani ili kuwabaini," alisema Chifuno.

Hata hivyo, mameneja wa mapori hayo walisema kuwa mbali na changamoto hizo kumekuwa na msako wa majangili ambao umekuwa ukihusisha ndege ambayo imekuwa ikiruka kwa nyakati tofauti katika mapori hayo.

Vilevile walisema ndani ya mapori hayo kuna vikosi kazi vya askari ambavyo vimepewa mafunzo maalumu ya kukabiliana na majangili.



Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), mkoa wa Mbeya, wakikagua mradi wa maji katika Halmashauri ya Busokelo, wilayani Rungwe, hivi karibuni. **PICHA: INNOCENT NG'OKO**

# Watanzania watajwa uvivu kusoma vitabu

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

WATANZANIA wametajwa kutokuwa na utamaduni wa kujisomea vitabu kwenye maktaba, badala yake wamekuwa wakijisomea kwa kufuata matukio ikiwamo wakati wa mitihani na kujiendeleza kielimu.

Kauli hiyo imetolewa na Mkutubi wa Maktaba ya Mkoa wa Mbeya, Justin Lwambo, wakati akizungumza na Nipashe na kueleza kuwa katika maktaba ya Mkoa wa Mbeya wamekuwa wakipokea idadi ndogo ya wananchi licha ya kuwahamasisha kujenga utamaduni wa kujisomea vitabu.

Alisema idadi ya watu wazima ambao wamekuwa wakijisomea vitabu ni ndogo ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi ambao wamekuwa wakijisomea katika maktaba hiyo kwa nyakati tofauti mkoani Mbeya.

Lwambo alisema kwa sasa wanaendelea na mikakati mbalimbali ya kuijenga jamii kuwa na utamaduni wa kupenda kujisomea katika maktaba mbalimbali zilizopo hapa nchini.

Alisema kwa Mkoa wa Mbeya wamefanikiwa kujenga maktaba ya watoto ambao hufika na kuweza kujisomea.

"Serikali imefanikiwa kujenga jengo la watoto wadogo kwa Mkoa wa Mbeya kwa lengo la kuwapa nafasi watoto wadogo kuweza kujisomea pamoja na kuwajengea utamaduni wa kuwa na utaratibu wa kupenda kijisomea hata watakapo kuwa wakubwa," alisema Lwambo.

Alisema kuwa kuna mkakati wa kuhakikisha kunakuwa na maktaba katika ngazi za wilaya na kata mkoani humo kwa kushirikiana na halmashauri husika kwa lengo la kuiwezesha jamii kupata maarifa.

Lwambo alisema kuna baadhi ya mikoa imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuanzisha maktaba hizo ukiwamo Mkoa wa Iringa na Kagera na kupata mafanikio.

Alisema maktaba hiyo imekuwa ikishirikiana na shule mbalimbali za Mkoa wa Mbeya kwa lengo la kuwahamasisha wanafunzi kuwa na utamaduni wa kujisomea na kuongeza maarifa yao ya kila siku.

Alisema katika siku zijazo wanakusudia kutoa huduma ya maktaba kwa njia ya Teknolijia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) na changamoto iliyopo upatikanaji wa vifaa.

# NHC kufanya operesheni ya wadaiwa sugu

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC) Mkoa wa Mbeya linakusudia kuendesha operesheni kwa wadaiwa sugu ambao hawajalipa kodi kwa muda mrefu.

Limesema kwa sasa linadai Sh. 16,009,999 ambazo zimesababishwa na wateja hao kuhama kinyemela na wengine kushindwa kulipa madeni wakiwa ndani ya nyumba hizo.

Kauli hiyo imetolewa na Meneja wa NHC katika mikoa ya Mbeya, Songwe na Njombe, Said Bungara na kueleza kuwa msako huo utafanyika kwa wapangaji wote walioshindwa kulipa madeni yao kwa mkoa wa Mbeya.

Alisema lengo la kukusanya madeni hayo ni kuiwezesha NHC kukusanya mapato zaidi kwa ajili ya maendeleo ya nchi ikiwamo kuwawezesha wananchi kupata huduma mbalimbali za kijamii.

"Niweke wazi tupo katika mchakato wa kukusanya madeni na kuingia makubaliano na wadaiwa namna ya kulipa madeni yao kabla ya hatua kali hazijachukuliwa dhidi yao ikiwamo kutaifisha mali zao," alisema Bungara.

Bungara alisema mpaka sasa NHC inaendelea na uhakiki wa wapangaji na kwamba lengo ni kuwabaini wapangaji ambao wamekuwa na utamaduni wa kuwapangisha watu wengine bila ya kufuata utaratibu kulingana na maelekezo ya shirika hilo.

Alisema mbali na ukaguzi huo NHC limekuwa likiendeleza jitihada za ujenzi wa nyumba na kwamba mpaka sasa limeshajenga nyumba katika Wilaya za Mbarali nyumba (20), Mkoa wa Songwe (20) na katika Halmashauri ya Busokelo nyumba (14), pamoja na nyumba 50 katika Mkoa wa Njombe.

Bungara alisema mpaka sasa nyumba zote zilizojengwa katika Wilaya za Mbarali na Halmashauri ya Busokelo zimeshanunuliwa na Halmashauri ya Mbarali na zile za Busokelo zimenunuliwa na halmashauri.

"Shirika limekuwa likijenga nyumba zenye ubora unaokidhi mahitaji ya wananchi na ndiyo maana nyumba nyingi zimekuwa na soko kubwa kwa taasisi za serikali na wananchi ambao wamekuwa wakizinunua muda mfupi tu baada ya kukamilika," alisema Bungara.

Alisema NHC limekuwa likiwauzia na kuwapangisha wananchi nyumba kwa bei ya chini kwa lengo la kukidhi mahitaji ya Watanzania kupanga katika shirika ambalo lipo nchini la serikali.



# Mahakama yakumbushwa wajibu maendeleo, uchumi wa viwanda

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KUTOKANA na azma ya serikali ya kuwa na uchumi wa viwanda, Mahakama imetakiwa kuhakikisha sheria zinazochochea azma hiyo zinapata tafsiri sahihi.

Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma, Mustafa Siyami, alisema jana jijini hapa kuhusu Siku ya Sheria, huku akisisitiza kuwa mahakama ina mchango mkubwa kuhakikisha sheria zinapata tafsiri sahihi na mashauri mbalimbali ya kibiashara yanasikilizwa haraka.

"Mwaka huu kaulimbiu ni: 'Uwekezaji na Biashara ni Wajibu wa Mahakama na Wadau Kuweka Mazingira Wezeshi ya Uwekezaji'. Kauli hii inalenga ule mfumo wa sheria ili ufanye kazi maendeleo yapatikane, vyombo vinavyosimamia sheria vina wajibu fulani," alisema.

"Tunaposema nchi ya viwanda mahala popote hakukosekani na migongano ambayo huwa inaishia mahakamani. Migogoro ya kibiashara hutokana na uwekezaji mbalimbali uliofanyika," alisisitiza.

Jaji huyo alisema eneo ambalo uchumi unakua, migogoro ya kisheria ni mambo ya kawaida kutokea. "Wadau wa mahakama wana wajibu gani kuhakikisha uwekezaji unafanyika na uchumi unakua. Ule mchango wa mahakama na wadau wake ndio kaulimbiu yetu ya uwekezaji," alisema.

Kuhusu Siku ya Sheria, alisema kutakuwa na wiki ya sheria ambapo mambo mbalimbali yatafanyika ikiwamo maonyesho ya taasisi zinazoshirikiana na mahakama ili kutoa elimu za kisheria kwa wananchi.

"Hii ni fursa kwa wananchi kupata taarifa za mambo yanayofanyika na kupata msaada wa kisheria kupitia taasisi zinazotoa msaada wa kisheria," alisema.

Alisema kilele cha maadhimisho hayo kitafanyika jijini Dar es Salaam Februari 6, mwaka huu, na Rais John Magufuli atakuwa mgeni.

"Kuanzia Januari 31 hadi Februari 5, mwaka huu kutakuwa na maonyesho Viwanja vya Nyerere kwa ajili ya kutoa elimu na msaada wa kisheria," alisema.

Jaji huyo alisema wiki hiyo itaambatana na matukio mbalimbali ikiwamo kuzindua jengo la Mahakama ya Wilaya ya Kondoa, Mahakama ya Mwanzo Bereko na Iguguno.



Wakazi wa Mtaa wa Vikonje 'B', Kata ya Mtumba, jijini Dodoma, wakizungumza na waandishi wa habari jana, wakiwalalamikia viongozi wa kata hiyo kwa kutaka kuwaondoa kwenye maeneo wanayoishi kupisha mradi wa ujenzi wa nyumba za serikali.
**PICHA: PETER MKWAVILA**

# Sumu kuvu yadaiwa chanzo cha saratani

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesema madhara makubwa yanayosababishwa na uwepo wa sumu kuvu katika mahindi na karanga ni kansa ya ini pamoja na udumavu kwa watoto.

Hayo yalibainishwa na Mratibu wa Mradi wa Kudhibiti Sumu kuvu katika maeneo mbalimbali nchini (Tanipac), Chrispin Josephat, wakati akizungumza na gazeti hili kuhusiana na mikakati waliojiwekea katika kupambana na tatizo hilo.

Josephat alisema sumu kuvu ni hatari na inasababishwa na wakulima kutofuata taratibu na kanuni za kilimo katika maeneo au mikoa ambayo imeathiriwa na tatizo hilo.

"Kuna uhusiano wa kansa ya ini na chakula kilichoathiriwa na sumu kuvu ndio maana unaona serikali iko mstari wa mbele kuhakikisha inamaliza tatizo hilo hapa nchini," alisema Josephat.

Alisema saratani inashabihiana na usababishwaji wa uwepo wa sumukuvu katika mazao husussani mahindi na karanga.

Pia alisema sumu kuvu husababisha udumavu kwa watoto na kwamba mtoto akipata tatizo hilo, si rahisi kumrejesha katika ukuaji wake wa kawaida.

"Ninaomba wakulima na wasindikaji tuwe na utamaduni wa kufuata kanuni. Hii itasaidia kupunguza tatizo la sumu kuvu," alisema.

Pia alisema kutokana na hali hiyo, mkataba wa miaka mitano ambao serikali imetia saini hivi karibuni, utatatua changamoto katika mikoa ambayo imeathiriwa na sumu kuvu kwa kiasi kikubwa.

"Tunakwenda kuboresha miundombinu bara na visiwani ikiwemo kutoa elimu. Lengo ni kutokomeza kabisa tatizo hili," alisema Josephat.

Alisema katika uboreshaji wamepanga kujenga maabara kubwa ya kimataifa yenye uwezo wa kupima mazao kabla ya kwenda nje hasa ukizingatia Tanzania inahudumia nchi nyingi katika suala la mazao.

Pia alisema wanatarajia kujenga maghala makubwa Tanzania Bara na Visiwani ambayo yatakuwa mfano wa kufundisha wakulima, wasindikaji jinsi ya kuhifadhi mazao yasiathiriwe na sumu kuvu.

Alisema pia wataanzisha na kuhamasisha matumizi ya vihenge vya kisasa ambavyo teknolojia zake zinatengenezwa na vijana nchini. Vihenge hivyo, alisema wanaamini vitakuwa msaada mkubwa kwa wakulima na wasindikaji wa mazao.

# Waziri Jafo aonya majungu

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amesema anasikitishwa na tabia ya watu wanaopeleka taarifa za uongo kwake ili kuwachongea wenzao wafukuzwe kazi au waondolewa kwenye nyadhifa walizo nazo.

Kauli hiyo aliitoa jana wakati akizungumza kwenye uzinduzi wa ofisi ndogo ya Jumuiya ya Serikali za Mitaa Tanzania (Alat) uliofanyika jijini hapa.

Jafo alisema anasikitishwa na tabia ya wafanyakazi hao ambao lengo lao ni kutimiza maslahi yao binafsi.

"Ndugu zangu naomba nieleze ukweli leo (jana). Nilikuwa nisije kuzindua jengo hili kutokana na maneno niliyoletewa na watu kuwa kuna ufisadi wa kutisha umefanyika kwenye ujenzi wa jengo dogo hili. Niliambiwa mtendaji mkuu ameiba ndoo za rangi na mabati amepakia kwenye basi la Machame. Kwa kweli nilikasirishwa sana," alisema Jafo.

"Pia niliambiwa hata jengo lenyewe haliwezi kukamilika kutokana na wizi uliofanyika na nikiambiwa kuwa viongozi wa juu wa Alat wanajilipa fedha na hawaendi kutembelea miradi ya halmashauri. Ilinibidi kuanza kuyafanyia kazi maneno haya haraka na nimegundua kuwa ni majungu ya watu," alisema.

Jafo alisema baada ya kusikia taarifa hizo, aliunda tume iliyoongozwa na Katibu Mkuu wa Tamisemi, Mhandisi Joseph Nyamhanga, ili kuchunguza na kujiridhisha juu ya tuhuma hizo.

Alibainisha kuwa baada ya kuunda, tume hiyo ilifanya kazi bila kuwahusisha viongozi wa Alat na ilijiridhisha pasipo na shaka kuwa taarifa hizo ni za uongo na hakuna hata fedha iliyoibwa.

"Tume ilijiridhisha na kubaini kuwa mtendaji mkuu anayepigwa majungu, aliziba mianya ya wizi na watu waliokuwa na lengo la kuibia Alat hasa wenye malipo ya kazi zilizokuwa zikifanyika kwenye ujenzi huu," alisema.

"Leo hii ningeambiwa kuwa taarifa hizo za wizi ni kweli, ningemfukuza kazi leo na kuagiza kufunguliwa mashtaka mtendaji mkuu kwa sababu hatupendi waturudishe nyuma katika maendeleo," aliongeza.

Pamoja na kuambiwa juu ya jengo kutokamilika, alisema alishangaa alipofika kuona limekamilika na kuanza kuamini kuwa taarifa hizo zilikuwa majungu ya watu wenye kutamani vyeo vya wengine kwa kupandikiza maneno ya uongo.



## Uhusiano Tanzania, Uturuki wahimizwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi, amesema Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Uturuki zina uhusiano wa kihistoria, ambao wawekezaji wa pande hizo mbili wanapaswa kuutumia kwa kushirikiana katika miradi ya kiuchumi ili kuudumisha.

Balozi Iddi alitoa kauli hiyo jana Mjini Zanzibar alipofanya mazungumzo na ujumbe wa viongozi waandamizi wa Kampuni za kimataifa za GÖKYOL na DAYK kutoka Uturuki waliofika nchini kuangalia maeneo wanayoweza kuwekeza katika nyanja ya miundombinu ya ujenzi.

Alisema mataifa mengi ulimwenguni yamekuwa na uhusiano wa kidiplomasia kwa miaka mingi baada ya uhuru, ambapo kwa sasa uhusiano huo unastahiki kuelekezwa zaidi kwenye diplomasia ya kiuchumi itakayoweza kusaidia kustawisha maisha na maendeleo ya wananchi wengi.

Aliushauri uongozi wa kampuni hizo kutenga muda mahsusi utakaowapata wasaa mpana zaidi wa kuangalia maeneo yanayostahiki kuwekezwa na kampuni zao zilizoanza kuonyesha azma ya kutaka kutumia fursa zilizopo nchini.

Alisema Zanzibar na Tanzania kwa ujumla zimekuwa na maeneo mengi yenye ushawishi wa kuimarishwa miundombinu yake hasa katika sekta ya ujenzi na mawasiliano yenye kuchukuwa nafasi kubwa ya ukuzaji uchumi wake kupitia bidhaa zinazotokana na sekta ya kilimo zinazostahiki kuingia katika soko.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Zanzibar, Mustafa Aboud Jumbe, alisema zipo barabara zisizopungua 11 katika maeneo mbalimbali ya visiwa vya Unguja na Pemba ambazo zimeshafanyiwa uchambuzi yakinifu zikisubiri fedha kwa ajili ya ujenzi wake.

Jumbe alisema serikali kupitia wizara hiyo iko tayari kushirikiana na wadau wa maendeleo katika kuona barabara hizo zenye urefu wa kilomita 150 zinajengwa na kutoa huduma nzuri.

Kwa upande wa sekta ya usafiri wa baharini, alisema jitihada zinaendelea kuchukuliwa katika kutafuta mbinu za kuipanua Bandari ya Malindi ili iwe na uwezo wa kutoa huduma kwa meli kubwa za mizigo zaidi ya moja kwa wakati mmoja.

Viongozi hao waandamizi wa GÖKYOL na DAYK walisema kampuni zao zilizoasisiwa miaka ya 1961 na 1971, zina uzoefu wa kimataifa katika ujenzi wa miundombinu ya barabara kuu na majengo ya hospitali na shule.

# Tamwa yaja juu dhamana kigogo anayedaiwa kubaka

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa) Ofisi ya Zanzibar, kimesikitishwa na uamuzi uliochukuliwa na Mahakama Kuu kumpa dhamana mtendaji mkuu wa Shirika la Biashara la Taifa la Zanzibar ZSTC Wilaya ya Mkoani Pemba, Seif Suleiman Kassim, hivi karibuni anayetuhumiwa kumbaka mwanafunzi.

Mkurugenzi wa Tamwa Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema mtuhumiwa huyo anatuhumiwa kumbaka mtoto wa kike wa miaka 13, mkazi wa Mkoani Pemba.

Kwa mujibu wa Sheria za Zanzibar hasa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Namba 7 ya Mwaka 2018 kifungu na 151, kubaka ni kosa ambalo halistahili kupewadhamana.

Alisema miongoni mwa sababu zilizomtoa nje kwa dhamana mtuhumiwa huyo ni kuwa ni mkurugenzi mtendaji wa ZSTC.

Alieleza kuwa Jaji anayesikiliza kesi hiyo alinukuliwa akisema kuwa ikiwa mtuhumiwa ataendelea kukaa rumande katika msimu huu, kutaathiri shughuli za uvunaji wa zao la karafuu.

"Tunaamini kwamba ZSTC ni shirika kubwa na lenye wafanyakazi wa kutosha wanaoweza kuzalisha hata pale ambapo mmoja au wawili katika wafanyakazi wake watakuwa hawapo kazini au hawafai kuendelea na kazi," alisema Dk. Mzuri.

Alieleza kuwa hoja ya dhamana ya mtuhumiwa wa ubakaji kwa sababu kama hiyo haitoshi na inaweza kuweka mfano mbaya katika mfumo wa haki.

Alieleza kuwa uamuzi huo haukuangalia upande wa pili wa waathirika au jamii kwa ujumla itajisikiaje itakapoona kuwa wapo watu wanapewa dhamana kutokana na nyadhifa zao japo kuwa kosa walilolitenda kisheria haliruhusiwi kupewa dhamana.

Dk. Mzuri aliviomba vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria kuzidisha umakini katika kutoa maamuzi kwa kuzingatia haki za binadamu na kuona kwamba haki ni lazima ifuate mkondo wake bila kujali cheo alichonacho mtu hata kama hakuna sheria inayompa kinga.

"Tunaiomba pia serikali kuingilia kati jambo hili kwa maslahi mapana ya kutekeleza mpango wa kitaifa wa kupambana na ukatili wa kijinsia (2017-2022) na jitihada za kuleta usawa wa kijinsia," alisema.



Waziri wa Afya Zanzibar, Hamad Rashid Muhammed (kushoto), akizungumza na Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Tanzania, Dk. Moha Damaj, wakati wa mkutano wa viongozi wa dini kuhusu masuala ya afya ya jamii, mjini Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ yaombwa wataalamu zaidi ushauri nasaha

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imeshauriwa kuongeza ajira za wataalamu wa ushauri nasaha ili jamii iweze kuondokana na matatizo mbalimbali yanayosababishwa na msongo wa mawazo.

Hayo yalielezwa jana na mtaalamu wa masuala ya ushauri nasaha, Asya Saleh Abdulkadir, wakati akizungumza na Nipashe.

Alisema jamii inakabiliwa na msongo wa mawazo kutokana na matatizo ikiwamo kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji.

Alisema ili nchi iendelee, lazima afya za watu kiakili ziwe sawa, hivyo ni vyema serikali kutoa fursa za ajira kwa wataalamu wa ushauri nasaha.

Aidha, alisema kuwa ipo haja kutolewa elimu ya ushauri nasaha kwa watoto wanaokaribia kubalehe au kuvunja ungo ili watoto hao waweze kuepukana kufanya vitendo vya udhalilishaji.

"Muda wa kubalehe au kuvunja ungo kwa watoto huwa wanakumbana na vishawishi vingi, hivyo ni vyema kupewa elimu ya ushauri nasaha ili kuvishinda vishawishi hivyo," alisema.

Asya alisema elimu ya ushauri nasaha ni muhimu hasa kwa wanafunzi shuleni kwa sababu wanakabiliwa na changamoto nyingi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Chuo cha Afya Zanzibar, Aziza Hamed, alisema wanatoa taaluma ya saikolojia baada ya kugundua kuwa jamii inakabiliwa na tatizo la msongo wa mawazo, hali ambayo inawafanya kufanya matukio mabaya.

Alisema ipo haja elimu ya saikolojia kutolewa kwa wanafunzi wa shule wanaofanya mitihani ya taifa ili kuweza kuyapokea matokeo ya mitihani yao katika hali nzuri.

"Yapo matukio ya wanafunzi kujiua baada ya kupata matokeo mabaya katika mitihani yao... kama wanafunzi wangekua wanapatiwa elimu ya saikolojia kabla ya kufanya mitihani, wasingekuwa wanafanya maamuzi mabaya baada ya kutopata matokeo mazuri," alisema.

Aidha, alisema chuoni hapo wamefungua kitengo cha ushauri nasaha, hivyo ameitaka jamii kufika chuoni hapo kupata ushauri nasaha pale wanapokutwa na matatizo.

Ofisa ustawi wa jamii Wilaya ya Magharib 'A' Unguja, Sabra Ali, alisema wanapokea kesi nyingi za watoto wanaokinzana na sheria ambapo watoto hao huwafanyia watoto wenzao vitendo vya udhalilishaji.

Alieleza kuwa watoto kama hao wanahitaji elimu ya ushauri nasaha ili wasirejee tena kufanya vitendo hivyo, lakini wilayani hapo hawana mtaalamu wa ushauri nasaha.

"Watoto kama hao huwa tunawapa ushauri nasaha, lakini hatuna utaalamu wa kutosha wa ushauri nasaha kwa sababu taaluma hiyo hatujasomea," alisema.

# Waliofaulu sekondari wapata shule

**Na Sabato Kasika**

KATIKA kuhakikisha wanafunzi wote waliochagulia kuanza kidato cha kwanza mwaka huu, shule mbili mpya za sekondari za kata za Busambara na Bugoji, Wilaya ya Musoma mkoani Mara, zimeanza kupokea wanafunzi hao.

Shule hizo ni Busambara Sekondari, iliyopo Kata ya Busambara, iliyoanza kupokea wanafunzi Januari 14 mwaka huu na Dan Mapigano Memorial School ya Kata ya Bugoji ilioanza kupokea wanafunzi Januari 16.

Mkuu wa Wilaya Musoma, Dk. Venvent Anney aliliambia gazeti hili kwa njia ya simu jana kuwa, hatua ya shule hizo kuanza kutoa masomo zinatokana na ushirikiano mzuri uliopo kati ya wazazi na serikali.

"Januari 14 wanafunzi 142 wa kidato cha kwanza wa Sekondari ya Busambara, walianza masomo, kwani wakazi wa vijiji vitatu vya Kwikuba, Maneke na Mwiringo walichangia nguvukazi na fedha," alisema Dk. Anney.

Alisema, kwa sasa sekondari hiyo ina walimu sita, ofisi mbili zenye meza, viti na kabati, vyoo vya wanafunzi matundu nane na vya walimu matundu mawili, kwamba kwa wakati huu vinatosha.

"Ujenzi wa maabara, madarasa mengine, maktaba, nyumba za walimu na viwanja vya michezo unaendelea, ili kuhakikisha shule hiyo inakuwa na miundombinu yote muhimu inayohitajika," alisema.

Kwa upande wa shule ya Dan Mapigano Memorial, mkuu huyo wa wilaya alisema, ilianza kupokea wanafunzi Januari 16 na kwamba wanafunzi wote 141 wa Kata ya Bugoji waliochaguliwa wameanza masomo.

Alisema, kabla ya kukamilika kwa sekondari hizo mbili, wanafunzi walikuwa wakisoma katika sekondari za kata za jirani, lakini sasa hao wa kidato cha kwanza wamepunguziwa kutembea umbali mrefu.

# Benki ya Azania yawakumbuka wajasiriamali

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Azania imeendelea kuwapa fursa mbalimbali wafanyabiashara wadogo, baada ya jana kuzindua huduma ya mikopo kwao.

Wafanyabiashara hao wamekuwa wakiwezeshwa na benki hiyo kwa njia mbalimbali zikiwamo kuwaletea bidhaa ambazo zitawakomboa kwa kuwaongezea mitaji pamoja na kuwawezesha kujitanua.

Hafla ya uzinduzi wa mikopo hiyo ya 'Jikwamue' ilifanyika katika eneo la soko la Mwaloni jijini Mwanza, ambapo mgeni rasmi alikuwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula.

Mikopo ya Jikwamue imezinduliwa ikiwa ni mwendelezo wa mkakati wa benki hiyo katika kuwainua kibiashara wajasiriamali wadogo sambamba na kuunga mkono jitihada za serikali ya Rais John Magufuli kuinua kipato cha mwananchi kupitia ujasiriamali.

Akizungumza katika uzinduzi wa mikopo hiyo Mkurugenzi Mkuu wa benki hiyo, Charles Itembe, alisema kuwa mikopo hii ni mahusus kwa ajili ya makundi mbalimbali ya kijamii ambayo katika masuala ya mikopo huwa yanashindwa kukidhi vigezo na masharti ya kukopesheka, makundi hayo ni kama kinamama, vijana, walemavu na makundi mengine maalum.

"Kupitia mikopo hii ya Jikwamue, mkopaji atajipatia mkopo bila kuweka dhamana yoyote, atahitaji tu kudhaminiwa na wanakikundi wenzake na kikundi kinaweza kukopeshwa hadi kufikia Sh. milioni 30 wakati mwanakikundi mmoja anaweza kukopeshwa hadi kufikia shilingi milioni 3, hivyo walengwa watahitaji kuunda kikundi cha wanachama wasiopungua watano hadi 10 ili kupata mkopo huu," aliongeza Itembe.

"Nadhani wote mtakubaliana na masharti haya ni nafuu sana na yanatekelezeka, hii itoshe kuonesha kuwa tunaposema tuna nia ya dhati katika kuwakomboa wafanyabiashara wadogo tunafanya hilo kwa vitendo. Sasa nitoe rai kwa kinamama, vijana, walemavu na makundi maalum kuchangamkia fursa hii adimu ili kujiongezea kipato na kukuza biashara na shughuli zenu maradufu," alisema Mkurugenzi huyo kauli ambayo iliwekewa msisitizo na Mwenyekiti wa Bodi ya wakurugenzi wa Benki hiyo, Mhandisi Julius Ndyamukamaa.

Ndyamukama aliwahakikishia wateja wa benki kuwa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki hiyo kuwa benki itaendelea kuisimamia vyema ili iendelee kutoa huduma zenye tija kama hii ya mikopo ya Jikwamue.

"Katika kuunga mkono kwa vitendo sera ya Rais John Magufuli ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati, ni lazima kuwa na mbinu za kuwaongezea wafanyabiashara wadogo kipato kupitia kufanyabiashara na benki zenye msingi imara... Benki ya Azania ipo tayari kushirikiana na wananchi na serikali katika kufanikisha hilo," aliongeza Mhandisi Ndyamukama.

Waziri Mabula aliipongeza menejimenti ya benki hiyo kwa kubuni huduma hii ambayo inawagusa Watanzania moja kwa moja. "Katika hili nikiri kuwa sisi kama serikali mmetuunga mkono kwa vitendo na mmeifanya kazi yetu ya kuwainua Watanzania kiuchumi izidi kuwa rahisi," alisema Mabula.

Mabula aliiomba benki hiyo kuendelea kutoa elimu ya ujasiriamali kwa wafanyabiashara wadogo ili kuwajengea uwezo wa kufanya biashara kwa weledi zaidi.




Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, mkoani Simiyu, Festo Kiswaga (kushoto), akipokea msaada wa meza na viti vya wanafunzi na walimu wa Shule ya Sekondari Ng'wang'wali, Kata ya Nyangokolwa, Halmashauri ya Mji wa Bariadi kutoka kwa Meneja wa Benki ya NMB, Kanda ya Magharibi, Sospeter Magesse, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampuni binafsi zapewa muda kujisajili kwa mfumo wa kisasa

**Na Mwandishi Wetu**

Jeshi la Polisi limezitaka kampuni binafsi za ulinzi kuhakikisha zimejisajili na kuwasajili walinzi wake kwenye Mfumo wa Uboreshaji wa Sekta ya Ulinzi Binafsi kwa njia ya kielektroniki (PSG-P), kwani baada ya Desemba 31, 2020 kampuni zote ambazo hazikutekeleza agizo hilo hazitaruhusiwa kufanya kazi nchini.

Akizungumza kwenye kipindi cha Kumekucha cha ITV, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Polisi, Narcis Missama, alisema mfumo huo unajumuisha kanzi data itakayokuwa na taarifa zote muhimu za kampuni binafsi za ulinzi zenye kibali halali cha kuwaruhusu kufanya shughuli za ulinzi nchini, wafanyakazi wa kila kampuni na taarifa zingine za wadau muhimu wa sekta hii wakiwamo watoa huduma zinazowezesha ufanisi wa sekta hii.

Alisema hatua ya kwanza ya usajili wa kampuni na wafanyakazi kwenye kampuni hizo inaendelea ambapo lengo la mfumo huo ni kuboresha sekta ya ulinzi, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa kila mlinzi anakuwa na sifa stahiki na amepata mafunzo yatakayoratibiwa au kutambuliwa na Jeshi la Polisi.

Pia, alisema mfumo wa PSG-P utarahisisha upatikanaji wa taarifa za mlinzi kwani kila mlinzi atakuwa na kitambulisho chenye namba maalum inayotolewa na Jeshi la Polisi kwa ajili ya kumtambulisha.

"Neno ambalo tunataka kulitoa kwa kampuni za ulinzi, na kwa hakika hata tukiwa nao huwa tunawaambia, ni kwamba tuhakikishe kila kampuni ifikapo mwishoni mwa mwaka huu iwe imejisajili kwenye mfumo huu. Kwa sababu baada ya hapo itakuwa imekwenda kinyume na makubaliano yetu yanayohusu uboreshaji na uimarishaji wa sekta ya ulinzi, lakini itakuwa imekiuka maelekezo yanayotolewa na Inspekta Jenerali wa Polisi ya usimamizi wa sekta hiyo ya ulinzi binafsi nchini," alisema Kamishna Msaidizi, Missama.

"Lakini neno lingine ni kwa walinzi wenyewe, wawahimize waajiri wao kuhakikisha kwamba wanawasajili kwenye mfumo huu kwani mlinzi ambaye atakuwa hajasajiliwa hataweza kupata ajira katika sekta binafsi ya ulinzi nchini. Lakini, ninapenda kuwaasa watumiaji wa huduma za walinzi binafsi kuwa ikishafika Desemba watafute huduma za ulinzi kwa kampuni ambazo zimesajiliwa na zenye walinzi ambao wako kwenye mfumo na taarifa za kampuni hizo zitapatikana kupitia tovuti itakayokuwa imeunganisha na mfumo wa PSG-P na kusimamiwa na Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyama vya kisekta," aliongeza. Jeshi hilo limeeleza kuwa baada ya usajili kila mfanyakazi hupewa kitambulisho chenye 'QR Code' hivyo kwa kutumia simu ya mkononi ya kisasa (smart phone) au kompyuta anaweza ku-scan na kuziona taarifa zote muhimu za mlinzi husika mara moja na hivyo kuwezesha utambuzi wao wa haraka.

Akizungumzia faida ya mfumo huo, ambao unatekelezwa kwa pamoja na vyama vya kisekta - TSIA na TAMASCA - chini ya usimamizi wa Jeshi la Polisi; Missama alisema kuwa pamoja na faida za kiusalama kwa kila anayetumia huduma, itasaidia kukuza uchumi wa nchi kwa kuwavutia zaidi wawekezaji kwani watakuwa na uhakika wa kupata huduma za ulinzi zenye viwango bora kupitia usimamizi na uratibu wa Jeshi la Polisi.

# TANGAZO

# TANDAHIMBA COMMUNITY BANK PLC

## UONYESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31/12/2019

(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | Mwaka ya /Mwaka wa 31/12/2019 | Mwaka/Uliopita 30/09/2019 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1. | Fedha Taslimu | 266 503 | 195 287 |
| 2. | Salio katika benki kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 | Uwekezaji katika amana za serikali | - | - |
| 4 | Salio katika benki nyingine na Taasisi za fedha | 1 105 509 | 568 118 |
| 5 | Hundi na miamala ya kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala baina ya matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizofikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za wateja zilizokubalilka | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa benki nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji katika amana nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo halisi iliyopo | 2 372 267 | 2 470 912 |
| 12 | Mali nyingine | 170 730 | 237 300 |
| 13 | Uwekezaji wa hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali zisizohamishika,mitambo na vifaa | 165 546 | 175 387 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | 4 080 555 | 3 647 004 |
| | | - | - |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za benki nyingine na Taasisi za fedha | - | - |
| 18 | Amana za wateja | 1 317 862 | 1 073 627 |
| 19 | Dhamana ya malipo kwa fedha taslimu | | |
| 20 | Amana Maalum | - | - |
| 21 | Maagizo ya malipo /Fedha kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za kibenki zilizotolewa | - | - |
| 23 | Iimbiko la kodi na ghalama zitakazolipwa | - | - |
| 24 | Dhima la tozo kwaajili ya usuluhishi baina ya benki na mteja | - | - |
| 25 | Fedha za washirika(MIVARF Grant) | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya kipindi kijacho na tozo nyingine zitakazo lipwa baadaye | - | - |
| 27 | Dhima nyingine | 8 751 | 158 479 |
| 28 | Madeni | 482 560 | 202 379 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **1 809 173** | **1 434 485** |
| **30** | **MALMI /(DHIMA) HALISI(16 kutoa 29)** | **2 271 382** | **2 212 519** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa hisa uliolipwa | 4 483 227 | 4 493 394 |
| 32 | Akiba ya mtaji | (2 394 634) | (2 410 480) |
| 33 | Mapato yaliyobakizwa | 64 550 | (16 863) |
| 34 | Faida(hasara)ya kipindi husika | 118 239 | 130 624 |
| 35 | Akaunti nyingine za mtaji | - | 15 844 |
| 36 | Stahiki za wenye hisa chache | - | - |
| **37** | **JUIMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **2 271 382** | **2 212 519** |
| 38 | Dhima zisizo dhahiri | - | - |
| 39 | Mikopo chechefu | 176 223 | 186 203 |
| 40 | Tengo kwa ajili ya mikopo chechefu | 65 412 | 64 428 |
| 41 | Mali nyingine chechefu | - | - |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I) | Uwiano wa fedha za wanahisa na jumla ya mali | 56% | 61% |
| (ii) | Uwiano wa mikopo chechefu na jumla ya mikopo ghafi | 7% | 7.5% |
| (iii) | Uwiano wa mikopo ghafi na jumla ya amana | 180% | 230% |
| (iv) | Uwiano wa mikopo halisi na jumla ya mali halisi | 58% | 68% |
| (v) | Uwiano wa mali zinazozalisha na jumla ya mali | 85% | 83% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 23% | 32% |
| (vii) | Ongezeko la mali | 12% | 5% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO INAYOISHIA 31/12/2019

(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | Robo ya mwaka wa sasa 31/12/2019 | Robo ya mwaka linganishi(Mwaka uliopita ) 31/12/2018 | Limbikizo la mwaka wa sasa 31/12/2019 | Limbikizo la mwaka linganisha (mwaka uliopita) 31/12/2018 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mapato yariba | 132 283 | 164 268 | 475 272 | 445 519 |
| 2. | Gharama za riba | (3 267) | (4 240) | (12 509) | (46 438) |
| 3. | Mapato halisi ya riba(1 kutoa 2) | **129 016** | **160 028** | **462 763** | **399 081** |
| 4. | Madeni viza yaliyopitwa | | | | |
| 5. | Punguzo/ongezeko la tengo katika mikopo | (983) | 13 350 | (8 353) | 3 940 |
| **6.** | **Mapato yasiyo ya riba** | **76 349** | **44 532** | **206 211** | **321 079** |
| | 6.1 Faida/(hasara) zitokanazo na miamala ya fedha za kigeni | - | - | - | - |
| | 6.2 Ada na kamisheni | 76 349 | 44 532 | 206 211 | 321 079 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato mengine | - | - | - | - |
| **7.** | **Gharama zisizo na riba** | **(122 968)** | **(146 840)** | **(596 070)** | **(627 999)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 14 685 | (24 194) | (236 506) | (261 009) |
| | 7.2 Ada na kamishani | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama nyingine | (137 653) | (122 646) | (359 564) | (366 990) |
| 8. | **Faida/(Hasara) ya uendeshaji** | **81 414** | **71 070** | **64 551** | **96 101** |
| 9 | Tengo la kodi ya mapato | (24 424) | (21 321) | (19 365) | (28 830) |
| **10** | **Faida /(Hasara)Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **56 990** | **49 749** | **45 186** | **67 271** |
| **11** | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa(bainisiha)** | | | | |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | | | | |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 15 | 15 | 15 | 15 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 18.16 | 16 | 14 | 21 |
| 14 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | | - | - | - | - |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | (I ) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 2.0% | 1.5% | 1.6% | 2.1% |
| | (ii) Uwiano wa Faida Baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 3.6% | 3% | 3% | 4% |
| | (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo na Riba na Mapato Ghafi | 60% | 72% | 89% | 87% |
| | (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 5% | 5% | 20% | 14% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHAKWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31/12/2019

(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | Robo mwaka ya sasa 31/12/2019 | Robo Mwaka iliyopita 30/09/2019 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31/12/2019 | Limbikizo la mwaka Linganishi(Mwaka Uliopita) 31/12/2018 |
|---|---|---|---|---|---|
| **I:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 64 550 | (16 863) | 64 550 | 96 101 |
| | Marekebisho Kwa Ajili ya: | 16 865 | 4 099 | 17 284 | (26 097) |
| | - Hasara Katika Mali | 9 840 | 5 823 | 31 281 | 50 823 |
| | - Badiliko halisi katika Mikopo | 98 644 | 49 245 | 575 520 | (1 077 710) |
| | - Faida/Hasara kwenye mauzo ya mali | - | - | - | - |
| | - Mabasiliko halisi katika amana | 244 235 | 257 854 | 225 205 | (3 071 046) |
| | - Mabadiliko halisi katika amana za muda mfupi zilizo afikiwa | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | (149 728) | (14 085) | (309 370) | 185 520 |
| | - Mabadiliko halisi katika mali nyingine | 66 570 | 62 235 | 42 906 | (2 537) |
| | - Kodi iliyolipwa | - | - | - | - |
| | - Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika)kwa shughuli za uendeshaji** | **350 976** | **348 308** | **647 376** | **(3 844 946)** |
| **II:** | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | | | |
| | gawio lililopokelewa | - | - | - | |
| | Ununuzi wa mali za kudumu | - | - | (19 411) | (114 124) |
| | Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | | | - | |
| | Ununuzi wa amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - | 0 | 0 |
| | Mapato kutokana na mauzo ya amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | |
| | Mengineyo (Bainisha) | | | - | 0 |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji** | **-** | **-** | **(19 411)** | **(114 124)** |
| **III:** | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha** | | | | |
| | Ulipaji wa madeni ya muda mrefu | - | - | - | |
| | Mapato kutokana na utoaji wa madeni ya muda mrefu | - | - | - | |
| | Mapato kutokana na utoaji wa mtaji wa hisa | (10 166) | 5 992 | (15 129) | 3 388 222 |
| | Gawio lilololipwa kwa fedha taslilmu | - | - | - | |
| | Mabadiliko halisi katika madeni mengine | 280 181 | (30 324) | (300 904) | (250 439) |
| | Mengnineyo | (12 384) | (23 397) | (138 188) | (88 633) |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(Zilizotumika) kwa shughuli za kifedha** | **257 631** | **(47 729)** | **(454 221)** | **3 049 150** |
| **IV:** | **Fedha taslimu na mali zinazo fanana na fedha taslimu** | | | | |
| | Ongezeko/Punguzo halisi kaitka fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslilmu | 608 607 | 300 579 | 173 744 | (909 920) |
| | Fedha na mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa robo mwaka/Mwaka | 763 404 | 462 825 | 3 526 118 | 5 189 006 |
| | **Fedha na mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa robo mwaka/Mwaka** | **1 372 011** | **763 404** | **3 699 862** | **4 279 086** |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHA 31/12/2019

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | ziada ya kisheria | Tengo la ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Robo Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa Robo mwaka wa sasa | 4 493 394 | 0 | -2 427 344 | 12 116 | 15 845 | 118 508 | 2 212 519 |
| Faida/(hasara) halisi baaada ya kodi ya mapato | | | 64 550 | | | | 64 550 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | | | 0 |
| Miamala na wanahisa | -10 166 | | 0 | | 0 | | -10 166 |
| Gawio lililolipwa | | | 0 | | | | 0 |
| Ziada ya kisheria | | | 0 | 0 | | | 0 |
| Tengo la ziada ya jumla | | | 15 845 | | -15 845 | 0 | 0 |
| Mengineyo | | | 16 865 | | 0 | -12 387 | 4 478 |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka** | 4 483 228 | 0 | -2 330 084 | 12 116 | 0 | 106 121 | 2 271 381 |
| **Robo ya Mwaka iliyopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo mwaka** | 4 487 402 | 0 | -2 414 844 | 12 116 | 15 845 | 141 905 | 2 242 424 |
| Faida/(hasara) halisi baaada ya kodi ya mapato | | | -16 863 | | | | -16 863 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | | | 0 |
| Miamala na wanahisa | 5 992 | | 0 | | 0 | | 5 992 |
| Gawio lililolipwa | | | 0 | | | | 0 |
| Ziada ya kisheria | | | 0 | 0 | | | 0 |
| Tengo la ziada ya jumla | | | 0 | | 0 | 0 | 0 |
| Mengineyo | | | 4 363 | | 0 | -23 397 | -19 034 |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka** | 4 493 394 | 0 | -2 427 344 | 12 116 | 15 845 | 118 508 | 2 212 519 |

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha ,sera za uandaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

**Tarehe**

Mugwagi Steven — 30/01/2020
**Mtendaji Mkuu**

Anthony Bichakila — 30/01/2020
**Mkuu wa fedha**

**Sisi,tuliotajwa hapo chini ,wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu ,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Benki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006,na zinaonesha hali halisi.**

**Tarehe**

Mohamed Mwinguku — 30/01/2020
Mwenyekiti wa bodi

Juma Namuna — 30/01/2020
Mjumbe wa bodi

# VALENCIA YAIFUNGULIA MLANGO BARCA KWA RODRIGO




**VALENCIA,** Hispania

KOCHA wa Valencia, Albert Celades amesema majadiliano juu ya uhamisho wa Rodrigo Moreno kwenda Barcelona yapo "wazi".

Rodrigo alirudi kutoka chumba cha majeruhi Jumamosi wakati Valencia ikiichapa Barca 2-0 kwenye dimba la Mestalla, na kumfanya kocha, Quique Setien kupoteza mchezo wake wa kwanza tangu achukue nafasi ya Ernesto Valverde.

Huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania akikosa mazoezi Jumatatu kwa ajili ya kwenda kuchunguzwa maumivu yake ya goti mjini Barcelona, sasa uhamisho wa kwenda kwa mabingwa hao wa LaLiga upo wazi kwa mzaliwa huyo wa Brazil.

"Rodrigo ni mchezaji ambaye anaweza kutengeneza tofauti, ndio sababu Barcelona wanamtaka," alisema Celades akiviambia vyombo vya habari.

"Majadiliano yapo wazi na hatutaficha. Rodrigo na mimi tumezungumza. Siwezi kuyaweka hadharani majadiliano yetu."

Kuwasili kwa Rodrigo kutaipa nguvu Barca ambayo imempoteza Luis Suarez, ambaye ni majeruhi na anatarajiwa kuwa nje ya uwanja kwa miezi minne kutoka na majeraha ya goti.



# Manchester United kuwafungia maisha waliovamia kwa Woodward

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United itamfungia maisha shabiki yeyote ambaye atabainika kuhusika kwenye kuvamia nyumba ya Makamu Mwenyekiti wake Mtendaji, Ed Woodward, Jumanne wiki hii.

Gazeti la Mirror liliripoti kwamba mashabiki kati ya 20 na 30 walivamia nyumba ya Woodward kabla ya mchezo wa pili wa nusu fainali ya EFL dhidi ya Manchester City uliopigwa Jumatano.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari, klabu hiyo ya Ligi Kuu ilishutumu mashambulizi hayo, ikisema "hakutakuwa na msamaha" kwa shabiki yeyote aliyehusika.

"Klabu ya Manchester United usiku huu inafahamu kilichotokea nje ya nyumba ya mmoja wa waajiri wetu," ilisema taarifa hiyo.

"Tunajua kwamba dunia ya soka itaungana na sisi na itakuwa nyuma yetu, huku kazi kubwa ya polisi ikifanywa kwa ajili ya kuwatambua washukiwa.

"Mtu yeyote atakayepatikana na hatia hii ya jinai, au kukutwa na hatia ya kuingia kwenye mali za mtu mwingine bila ruhusa, atafungiwa maisha yake yote na klabu.

"Mashabiki kutoa maoni yao ni jambo moja, kufanya tukio la jinai kwa kuhatarisha maisha ya mtu au mali zake ni jambo jingine. Hakuna msamaha kwa hili."

Inadaiwa mashabiki wa Manchester United wanamuona Woodward kama chanzo cha timu hiyo kuvurunda.

# Kocha Aston Villa apagawa kutinga Kombe la Ligi

**LONDON,** England

DEAN Smith "atakuwa mtu mwenye fahari kubwa" wakati atakapoiongoza Aston Villa kucheza fainali ya Kombe la Ligi (EFL Cup) kwenye dimba la Wembley baada ya kuichapa Leicester City 2-1 kwenye mchezo wa nusu fainali ya pili, Jumanne.

Mchezo huo uliopigwa kwenye Uwanja wa Villa Park ulionekana kama ungeamuliwa kwa mikwaju ya penalti, wakati Kelechi Iheanacho aliposawazisha bao la Matt Targett na kufanya matokeo kuwa 1-1 na 2-2 kwa uwiano kufuatia mechi ya awali nayo kumaliza kwa kufungana 1-1.


Hata hivyo, Trezeguet alitumia vizuri krosi ya Ahmed El Mohamady (wote raia wa Misri) kufunga bao la ushindi katika dakika ya mwisho kabisa ya mchezo huo.

Villa, ambao kwa mara ya mwisho walishinda taji hilo mwaka 1996 na walikuwa washindi wa pili mwaka 2010, sasa watakutana na Manchester City ama Manchester United kutegemeana na matokeo ya jana baada ya timu hizo mchezo wa awali miamba hiyo ya Old Trafford kukubali kipigo cha mabao 3-1.

"Kwa uhakika hili lilikuwa lengo langu. Kuiongoza timu kwenye fainali pale Wembley, hakika ni fahari kubwa zaidi kwangu," alisema Smith akiiambia Sky Sports.

"Tulishinda kama ilivyotokea dhidi ya Watford katika dakika ya mwisho kabisa, hakika ni fahari kwangu."

Katika mchezo huo, Mtanzania Mbwana Samatta aliichezea timu hiyo kwa mara ya kwanza tangu ajiunge nayo wiki iliyopita kwa pauni milioni 10 akitokea KRC Genk ya Ubelgiji.



# MANE KUKOSA MECHI ZAIDI ZA LIVERPOOL



**LIVERPOOOL,** England

KOCHA Jurgen Klopp amethibitisha kwamba mshambuliaji wake, Sadio Mane ana uwezekano wa kukosa mechi mbili zaidi zijazo za Liverpool kutokana na kuendelea kuuguza misuli ya nyama za paja.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal, Mane alitolewa nje kipindi cha kwanza wakati Liverpool ikiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Wolves Alhamisi iliyopita baada ya kuumia misuli.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, hakuwapo kwenye mchezo wa sare ya 2-2 dhidi ya Shrewsbury Town katika mechi ya raundi ya nne ya Kombe la FA Jumapili na aliukosa mchezo wa jana Jumatano wa Ligi Kuu dhidi ya West Ham.

Hata hivyo, Klopp anamtarajia Mane kuukosa mchezo mmoja wa nyumbani dhidi ya timu yake ya zamani ya Southampton Jumamosi, huku akibainishwa kwamba hali yake si mbaya sana.

"Sadio hatacheza dhidi ya West Ham (jana) na pengine dhidi ya Southampton," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari Jumanne.

"Baada ya hapo atakuwa fiti, halafu wiki moja baada ya hapo atakuwa tayari kurudi uwanjani.

"Aliumia na sasa anaendelea vizuri, ingawa tumeamua abakie kwanza nje ya uwanja akiendelea kujiuguza, lakini tuna bahati kwamba majeraha yake si makubwa sana.

"Lakini wakati tukiwa na michezo mitatu ndani ya wiki inamaana atakuwa nje kwa mechi tatu."

Mane ameanza katika mechi 21 za Liverpool iliyocheza mechi 23 kwenye Ligi Kuu msimu huu na ametumika mara 31 kwenye mashindano yote.

## Fernandinho aongeza mwaka Man City



**MANCHESTER,** England

FERNANDINHO hataondoka Manchester City mwishoni mwa msimu huu baada ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil kuongeza mkataba wa mwaka mmoja.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, alionekana kama angeondoka Julai, wakati mkataba wake utakapomaliza, lakini City wamemhakikishia kwamba ataendelea kuwapo hapo angalau kwa msimu mmoja zaidi.

Kiungo huyo mtaalamu, Fernandinho alijiunga na City akitokea Shakhtar Donetsk mwaka 2013 na msimu huu amekuwa nguzo muhimu zaidi kwa timu hiyo kwenye safu ya ulinzi na akicheza angalau mechi 29 za Ligi Kuu karibia kila msimu.

Amebakia kuwa muhimu zaidi msimu huu, akicheza mechi 20 na kuwa beki wa kati kutokana na City kukumbwa na tatizo la majeruhi kwa walinzi wake.

"Ilikuwa rahisi," alisema akinukuliwa na tovuti ya klabu hiyo baada ya kusaini mkataba mpya na City.

"Kuna wakati katika maisha yako huwezi kujifikiria wewe mwenyewe tu, lakini hasa familia yako na watoto. Walikuwa moja ya sababu mimi kuamua kusaini mkataba wa mwaka mmoja zaidi.

"Nina furaha, familia yangu inafuraha, hivyo natumaini hata mashabiki wa City wanafuraha pia."

## *Fernandes: Kucheza EPL ni ndoto yangu*

**LISBON,** Ureno

BRUNO Fernandes amesema kuhamia kwenye Ligi Kuu ya England "mara zote" lilikuwa jambo muhimu zaidi kwamba, baada ya Manchester United kuripotiwa kwamba, imefikia makubaliano ya kumsajili nahodha huyo wa Sporting CP.

Usajili wa mchezaji huyo unaaminika kufikia mwisho, huku Fernandes akitarajia kuondoka Sporting kwenda United kwa ada ya awali ya pauni milioni 47 na utakamilika siku ya mwisho kesho ya kufungwa kwa dirisha dogo la usajili, Ijumaa.

Fernandes amekuwa akihusishwa kwa muda mrefu na wanaojikongoja kwenye Ligi Kuu United mwezi huu na madirisha yaliyopita, ameripotiwa kwamba alisafiri kwenda Manchester jana Jumatano.

Alipoulizwa kama kucheza Ligi Kuu ya England ndio kilikuwa kipaumbele chake zaidi baada ya kuhusishwa pia na kutakiwa na miamba wa LaLiga, Barcelona na Valencia, Fernandes aliiambia SIC: "Mara zote ilikuwa hivyo."

Fernandes, ambaye alikuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa kule Tottenham na Real Madrid, amefunga mabao 15 kwenye mashindano yote msimu huu akiwa na Sporting.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, alifunga mabao 31 msimu uliopita, yakiwamo 20 kwenye Ligi Kuu ya Ureno, Primeira Liga.

Kikosi hicho cha Ole Gunnar Solskjaer kitacheza na Wolves kwenye mchezo wa Ligi Kuu Jumamosi kabla ya kwenda mapumziko ya muda mfupi.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ALISSON AKIMBIZA KIWANGO MAKIPA EPL

●●● Kitakwimu anaruhusu bao moja kila dakika 214 sasa anyemelea rekodi ya Petr Cech...

**LONDON,** England

KIPA namba moja wa Liverpool, Alisson ndiye golikipa bora anayefanya vizuri zaidi kwenye Ligi Kuu ya England kwa mujibu Kampuni ya Takwimu za Magolikipa, Stats Perform Goalkeeper Index.

**Ukiangalia kitakwimu ambavyo amecheza mechi bila kuruhusu bao, mabao aliyofungwa na asilimia ya hatari alizookoa, kunamfanya kipa huyo kuifanya timu yake kuwa na safu yenye ulinzi imara zaidi.**

Kwa mashuti yaliyomlenga kunafanya vitu kusonga mbele na mlinganisho wa kiwango chake kuwa kama kipa wa 'wastani', lakini kwa kila hatari iliyoelekea langoni mwake ni ngumu kumlinganisha thamani yake.

Katika hatari ya mabao ya kuokoa yaliyoelekea langoni mwake, Vicente Guaita wa Crystal Palace ndiye golikipa anayefanya vizuri zaidi, akiokoa mabao 6.6 (sawa na dakika 29.6 kwa mabao 23 aliyofungwa, yakiwamo mabao ya kujifunga), huku Alisson ana tofauti ya 0.3 (sawa na kuokoa mabao 6.3).

Hata hivyo, katika takwimu hizo, zimemkadiria kila kipa na kwa namna gani shuti la aina moja linavyoweza kuokolewa.

Juu ya hilo inachukua historia ya uwezo wa kipa kuokoa hatari hasa yakiwamo mashuti kuelekea langoni mwake (kushoto, katikati au kulia kwa goli) na kwenye 'kona' ya juu na yale yaliyomlenga moja kwa moja.

Magolikipa wa Ligi Kuu ya England wamekabiliana na mashuti 2,108 msimu huu na takwimu zinaonyesha namna gani makipa walivyojitahidi kuokoa na yaliyoingia langoni mwao.

Ukiangalia kwa mchezo mmoja mmoja, pamoja na ulinganisho wa wastani kwenye ligi, matokeo yanakuwa wazi kabisa.

Alisson, ameokoa 0.58 ya mabao kwa mchezo ikiwa ni wastani mkubwa zaidi kwenye ligi na kunamfanya yeye kuwa kinara dhidi ya kipa wa Manchester City, Ederson aliyeokoa 0.27.

Msaidizi wa nahodha wa Tottenham, Hugo Lloris, Paulo Gazzaniga ana 0.16, David de Gea wa Manchester United, (0.16) na Bernd Leno wa Arsenal (0.13) akiwa anashika nafasi ya tano.

Kwa upande mwingine golikipa wa Southampton, Angus Gunn katika mechi 10, anatarajiwa kuruhusu 0.50 ya mabao kwa mchezo mmoja, ikiwa ni mabao zaidi ya wastani wa kwenye ligi.

Hivyo basi, Alisson anatarajiwa kuokoa 1.08 ya mabao kwa mchezo mmoja zaidi ya Gunn.

Kipa huyo wa kimataifa wa Brazil ameruhusu bao moja katika kila dakika 214 kwenye Ligi Kuu msimu huu.

Kama akiendelea na kiwango hiki, anaweza kuvunja rekodi ya Petr Cech ambaye aliruhusu bao moja kila baada ya dakika 242 kwenye Ligi Kuu.

## ZISIKUPITE

### BARCA YAIVURUGIA UNITED

BARCELONA imetoa ofa dakika za mwisho kujaribu kuizuia Manchester United kwenda kumsajili kiungo wa Sporting Lisbon, Mreno Bruno Fernandes, 24. ***(Mirror)***

### CHAMBO YA RODRIGO

BARCELONA imepanga kumsajili kiungo wa Sporting Lisbon, Mreno Bruno Fernandes, 24, na haraka kumtoa kwa mkopo Valencia ili kukamilisha dili la mshambuliaji wa Valencia, Mhispania Rodrigo, 28, lakini mazungumzo hayo yanakaribia kuvunjika. ***(ESPN)***

### ARSENAL, MATVIYENKO SAFI

ARSENAL Imekubaliana dili la kikanuni la kumsajili beki wa Ukraine, Mykola Matviyenko, 23, kutoka Shakhtar Donetsk. ***(Team1, via Metro)***

### WIJNALDUM NJIAPANDA LIVER

KIUNGO Mholanzi Georginio Wijnaldum, 29, amekiri kwamba hana uhakika endapo atabaki Liverpool msimu ujao. ***(Talksport)***

### GIROUD AWINDWA SPURS

SPURS pia imefanya mawasiliano na Chelsea ya kumsajili mshambuliaji wa kimataifa wa Ufaransa, Olivier Giroud, 33. ***(90min)***

### GOMEZ AGEUZIWA RADA UTD

MANCHESTER United tayari imemgeukia mshambuliaji wa Valencia, Maxi Gomez, 23, ambaye ana kipengele kinachomruhusu kuuvunja mkataba wake kwa pauni milioni 118.5, kuwa chaguo lake la kwanza katika usajili wa majira ya joto. ***(Cadena Ser - in Spanish)***

### KUIGHARIMU BARCELONA

ARSENAL haitamruhusu mshambuliaji wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang, 30, kuondoka chini ya pauni milioni 50, huku Barcelona ikivutiwa naye. ***(Express)***

### SHEFFIELD YAKOMA NA BERGE

SHEFFIELD United ni klabu pekee iliyotoa ofa kwa kiungo wa KRC Genk, Sander Berge, wakati mazungumzo yakiendelea ya kumnasa kwa pauni milioni 27. ***(Mail)***

### PIATEK AILILIA TOTTENHAM

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Poland, Krzysztof Piatek, 24, anataka kuondoka AC Milan na kujiunga na Tottenham kabla ya dirisha la usajili kufungwa. ***(Express)***

### LEMAR AMULIKWA BAYERN

BAYERN Munich imejiweka sawa na uwezekano wa kwenda kumsajili kiungo wa Atletico Madrid, Mfaransa Thomas Lemar, 24. ***(France Football)***

### ARSENAL BADO KWA MARI

ARSENAL bado imeendelea kuzungumza na Flamengo kuhusu uwezekano wa kumpata beki Mhispania Pablo Mari, 26. ***(ESPN)***

### BAYERN BADO INAYE SANE

MTENDAJI Mkuu wa Bayern Munich, Karl-Heinz Rummenigge amekataa kuweka kando uwezekano wa kwenda kumsajili winga wa Manchester City, Mjerumani Leroy Sane, 24. ***(Mirror)***

# HABARI MICHEZO

## Matumla kukuza ngumi Manyara

**Na Mwandishi Wetu**

BONDIA mkongwe wa hapa nchini, Rashid Matumla, amesema anajiandaa kuhamishia makazi yake katika mkoa wa Manyara ili kukuza na kufufua vipaji vya mabondia wa mkoani humo.

Matumla (pichani chini) aliamua kutoa ahadi hiyo baada ya kuona wakazi wa mkoa huo wameamua kuwekeza katika mchezo wa ngumu, ikiwamo kutengeneza jukwaa la kisasa.

Bondia huyo alisema kitendo cha mkoa kuingia gharama ya kutengeneza ulingo kwa ajili ya kufanyia mazoezi ya kila siku ni cha kupongezwa na ameweka wazi atashiriki katika kunyanyua mabondia wa mkoa huo.

"Ulingo ndiyo kila kitu, kwa sababu siku zote ukiona watu wanacheza Marekani pamoja na nchi zingine wanafanikiwa ujue unacheza kwenye ulingo, kama mkoa unakosa ulingo kwa kweli inakuwa hamna kitu, lakini wachezaji wanapata hamasa kutokana na kupatikana kwa vifaa bora," alisema Matumla.

Alisema pia hali ya hewa ya Manyara inaruhusu kufanya vizuri mazoezi na ametoa ombi kwa viongozi wa mkoa ili kupata kibali cha kuhamia mkoani hapo.





Wachezaji wa timu ya African Lyon, wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana kujiandaa na mchezo wa Ligi Daraja la Kwanza dhidi ya Mbeya Kwanza unaotarajiwa kuchezwa Jumamosi wiki hii. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# AZAM, MTIBWA SUGAR MECHI YA REKODI BARA

**Na Somoe Ng'itu**

SAFARI ya kuwania ufalme wa Tanzania inatarajiwa kuendelea leo kwa Azam FC kuwakaribisha Mtibwa Sugar katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Iddi Cheche, amesema timu yake imejiandaa kuendeleza kasi ya ushindi ili malengo yao ya kutwaa ubingwa wa msimu huu yatimie.**

Cheche alisema wanajua mchezo wa leo utakuwa na ushindani kwa sababu Mtibwa Sugar inaundwa na wachezaji wenye uzoefu na ligi hiyo huku pia wakiwa na vipaji vizuri. Alisema wataingia uwanjani kwa umakini na watajipanga kucheza kwa ubora ili waondoke na pointi tatu muhimu za mchezo huo.

"Tumemaliza mchezo wa FA, sasa nguvu zetu ni katika Ligi Kuu, tunajua mchezo huu utakuwa na ushindani mkubwa, Mtibwa Sugar ina wachezaji wenye uzoefu na vipaji, tunauchukulia uzito wake, tunaamini tutafanya vema," alisema Cheche.

Naye Ofisa Habari wa timu hiyo, Jaffer Iddi, alisema wanaomba mashabiki wao waendelee kuwaunga mkono na kufanya kwao vizuri kunatokana na ushirikiano wanaowapa.

"Tunafahamu umuhimu na ugumu wa mchezo huo, sasa hivi timu imeonyesha ina nguvu, inapambana kupata matokeo mazuri uwanjani, tunawashukuru mashabiki wetu, wao ndio chachu ya sisi kufanya vizuri, tunawaamini na tunasema shukrani sana," Iddi alisema.

Kocha Mkuu wa mabingwa hao wapya wa Kombe la Mapinduzi, Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, amesema kikosi chake kiko tayari kwa mchezo huo na wataingia kuikabili Azam FC kwa umakini zaidi.

"Tumeshaingia Dar es Salaam na tuko kamili kuelekea mechi hiyo, tumeangalia makosa yetu katika mechi iliyopita ya Kombe la FA, ili tusiyarudie, naamini ushindi utapatikana," alisema Katwila.

Katika msimamo wa ligi hiyo yenye timu 20, Mtibwa Sugar iko katika nafasi ya 10 ikiwa na pointi 22 baada ya kucheza michezo 16 huku Azam FC yenye pointi 35 ikiwa imeshuka dimbani mara 16 iko katika nafasi ya pili nyumba ya vinara Simba wenye pointi 41.



Wageni wa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Ackson, ambao ni viongozi wa Klabu ya Simba, kutoka kulia ni Ofisa Mtendaji Mkuu, Senso Mazingiza, Mkurugenzi wa Wanachama na Mashabiki, Hashim Mbaga, Ofisa Habari, Haji Manara na Ofisa Miradi wa klabu hiyo, Belinda Paul, wakiwa bungeni jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

## *Tanzanite yaenda Uganda kibabe*

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha timu ya soka ya Taifa ya Wanawake wa umri chini ya miaka 20, kinaondoka nchini leo kuelekea Uganda ili kuwakabili wenyeji wao katika mchezo wa kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia la Vijana zitakazofanyika baadaye mwaka huu nchini Panama.

Uganda wanatarajia kuwakaribisha Tanzanite katika mchezo wa marudiano utakaochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa KCCA, Lugogo jijini Kampala.

Kocha Mkuu wa Tanzania, Bakari Shime, alisema wanaenda katika mchezo huo kumalizia kazi waliyoianza hapa nyumbani na wamejipanga kukutana na ushindani kutoka kwa wenyeji wao.

Shime alisema Tanzania na Uganda zinafahamiana na mchezo huo wa marudiano unatarajiwa kuwa mgumu, lakini anaamini wachezaji wake watapeperusha vema bendera ya nchi.

Tanzania itashuka katika mchezo huo ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 2-1 walioupata katika mechi ya kwanza iliyochezwa Januari 19, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

# Michezo

Alhamisi Januari 30, 2020

Nipashe




Alisson akimbiza kiwango makipa EPL UKURASA 30



Beki wa Leicester City, Jonny Evans (kushoto), akiwa amemshika mshambuliaji wa Aston Villa, Mbwana Samatta kumzuia asilete madhara wakati beki mwenzake Caglar Soyuncu akiwa ameruka juu kuucheza mpira kwa kichwa kwenye mechi ya nusu fainali ya Kombe la Ligi iliyopigwa Uwanja wa Villa Park juzi usiku na wenyeji kushinda 2-1. **PICHA: MTANDAO**

## Arsenal sasa yamnasa beki kisiki, Pablo

**LONDON,** England

ARSENAL imekamilisha usajili wa beki kisiki, Mhispania Pablo Mari kwa mkopo huku kukiwa na kipengele kinachoipa nafasi ya kumnunua jumla mwishoni mwa msimu.

Mari, 26, anakuwa usajili wa kwanza kwa kocha Mikel Arteta tangu alipotwaa mikoba ya kuinoa timu hiyo Desemba mwaka jana baada ya beki huyo kutoka Flamengo kukamilisha usajili huo wa mkopo kwa pauni milioni nne.

Beki huyo alitua London Jumamosi akiwa na Mkurugenzi wa Ufundi wa Arsenal, Edu, ambaye alisifu Arsenal kukamilisha usajili huo.

"Pablo ni mchezaji mzoefu ambaye atatuongezea ubora katika safu ya ulinzi," Edu alisema wakati klabu hiyo ikithibitisha usajili huo.

"Tumekuwa tukifuatilia wasifu wa Pablo kwa kipindi na tuwenye furaha kufikia makubaliano na Flamengo kwa yeye kujiunga nasi awali hadi mwishoni mwa msimu. Pamoja na Mikel na benchi la ufundi tunatazama mbele kwa kumuona Pablo akiwa na jezi ya Arsenal."

# Samatta atusua, apewa bao

## ●●● Atuma salamu Manchester fainali Wembley, mabeki wa Leicester Evans na Soyuncu watajwa...

**Na Somoe Ng'itu**

KATUSUA! Hivyo ndivyo unavyoweza kusema baada ya nahodha wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars) na mshambuliaji mpya wa Aston Villa, Mbwana Samatta kufanikiwa kuchomoza katika kikosi cha kwanza cha timu hiyo ya Ligi Kuu England wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Leicester City juzi usiku, hivyo kutinga fainali ya Kombe la Ligi, EFL Cup.

**Samatta ambaye alikamilisha usajili wa kujiunga na timu hiyo Jumatatu ya wiki iliyopita akitokea Genk ya Ubelgiji, licha ya kutofunga katika mechi hiyo ya nusu fainali ya pili, mashabiki wa soka England na hapa nchini wamemzawadia bao lake la kuotea 'offside', lililokataliwa na refa wa mechi hiyo, Mike Dean.**

Katika mechi hiyo, ambayo licha ya Aston Villa kuzidiwa kimchezo, Matt Targett alianza kuifungia bao la kuongoza dakika ya 12 na kama si mshika kibendera kumuonyesha refa ishara ya Samatta kuotea, nahodha huyo wa Taifa Stars, angeweza kucheka na nyavu.

Hata hivyo, Kelechi Iheanacho aliisawazishia Leicester dakika ya 72 kabla ya mtokea benchi wa Aston Villa, Mahmoud 'Trezeguet' kuipeleka fainali timu yake kwa kuandika bao la pili katika dakika za majeruhi (90+2).

Hata hivyo, wachambuzi mbalimbali wameuelezea mwanzo wa Samatta kuwa mzuri huku wakilaumu mawinga wa pembeni wa Aston Villa kumbania pasi Mtanzania na jinsi alivyokuwa akijitafutia nafasi lakini wakashindwa kumlisha.

"Kuna wakati Jack Grealish alikuwa anaonyesha uchoyo kabisa, Samatta alipokuwa akiomba pasi, na namna nahodha huyo wa Stars alivyokuwa akicheza inawezekana kabisa ni maelekezo ya kocha.

"Unaona hata Jonny Evans na Caglar Soyuncu walikuwa wawili kwa mmoja dhidi ya Samatta, ambao nao walishindwa kuanzishia mpira katikati kwa kiungo Wilfred Ndidi kutokana na namna mshambuliaji huyo alivyokuwa amejipanga, na alipofanyiwa mabadiliko ndiyo Leicester walifunguka na mabeki kuwa huru kuipandisha timu kupitia Mnigeria huyo," alisema Emily Methew.

Kwa upande wa Samatta ambaye alicheza kwa dakika 65 katika mchezo huo, alisema: "Ushindi mkubwa tumepata jana (juzi) usiku na ninafuraha kwa nafasi niliyopata, mwonekano bora kutoka kwa mashabiki na kiwango kikubwa tulichokionyesha, sasa tunaelekea Wembley."

Na katika kuonyesha 'mahaba' kwa mchezaji huyo, mashabiki wa soka nchini wamediriki kusema wanalitambua bao la kuotea lililofungwa na mshambuliaji huyo wa zamani wa TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Simba na African Lyon (zamani Mbagala Market) zote za Tanzania.

Shabiki mwingine wa Samatta na mshambuliaji tegemeo wa Timu ya Taifa ya Uganda, Emmanuel Okwi alimtakia mafanikio zaidi nahodha huyo wa Stars: "Safi sana kaka," alisema kwa kifupi Okwi, mshambuliaji wa zamani wa Simba.

### MBAGALA YASIMAMA

Katika kuonyesha kwamba eneo la Mbagala lina historia na alama muhimu kwenye safari ya mshambuliaji huyo, maelfu ya mashabiki kutoka sehemu mbalimbali jijini walijitokeza kwa wingi kwenye Uwanja wa Shule ya Msingi Mbagala kutazama mechi hiyo ya kwanza ya Samatta kwa kutumia 'screen' kubwa iliyoandaliwa.

"Samatta alianzia katika uwanja huu, na mimi ndio nilikuwa nawapikia chakula, baada ya mazoezi ya pamoja, alikuwa akienda kufanya mazoezi mengine ya peke yake, nilimfichia chakula chake, akirudi ninampatia, kwa kweli alionyesha bidii tangu mapema akiwa mdogo," alisema mpishi huyo aliyejitambulisha kwa jina la Mama Mwita, huku akieleza Samatta amemuahidi zawadi.

Hata hivyo, mashabiki wengine kwa nyakati tofauti wamedai kwamba Samatta ameshindwa kufunga bao katika mechi yake hiyo ya kwanza kutokana na kutopewa pasi.

Katika kudhihirisha kiu ya mashabiki wa soka nchini ilikuwa ni kumuona Samatta akicheza, baada ya kufanyiwa mabadiliko katika dakika ya 65, baadhi ya mashabiki walianza kuondoka Mbagala na kwenye baadhi ya 'vibanda umiza', ambavyo Nipashe ilitawanya waandishi wake kufuatilia mchezo huo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >